

Nyumbani - Urafiki - Maji - Shamba

-Karama za Kiroho - Mkate - Vipawa - Dunia -

- Pesa - Ushuhuda - Wakati - Biblia - Elimu -

Iwe Nurur



MIMI NI

Mpumbavu Mwangalifu

Asiye Jali Mwema

Mwenye hekima

Mwovu Mwaminifu

Mvivu Tayari Mwongo

WAKILI

Jamaa - Hekima - Maisha - Mavazi

Iwe Nuru



MIMI NI WAKILI

**“Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo,
na mawakili wa siri za Mungu.**

**Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili,
ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu.”**

1 Wakorintho 4:1-2 (Union Version)

UWW 7-1-4

Bert Yates

©Copyright 1998

Kenya Baptist Media

P.O. Box 30370

Nairobi, Kenya

All rights reserved

Yaliyomo

Somo.....	Ukurasa
Utangulizi.....	4
1. Vitu Vyote Ni Vya Mungu.....	5
2. Wakili Mwema na Mwaminifu.....	9
3. Biblia Yetu na Uwakili.....	13
4. Uwakili wa Maisha Yangu	17
5. Wakati na Upendo Wangu kwa Mungu	21
6. Itumieni Miili Yenu kwa Ajili ya Kumtukuza Mungu	25
7. Mali Yangu na Moyo Wangu	29
8. Zaka na Dhabihu Zenu	33
9. Watoto Ni Zawadi Kutoka kwa Mungu	37
(Somo limeandikwa na Phyllis Maina)	
10. Karibuni Nyumbani Kwangu Mkakae.....	41
11. Wakili Mwema wa Karama za Kiroho	45
12. Ujumbe wa Kristo Ukae Moyoni Mwako	49
13. Mungu Afanye Madadiliko	53
Mpango wa Mungu wa Wokovu.....	Nyuma ya Kitabu

Utangulizi

Iwe Nuru ni mpango wa vitabu vya Wanawake Wabatisti wa Afrika ya Mashariki. Vinawezwa pia kutumiwa kama vitabu vya kujifunza kwa watu binafsi na makundi kama ya Ushirika wa Wanaume na vijana.

Masomo yaliyo katika kitabu hiki yanapaswa kutumiwa katika mikutano ya kila juma. Wakati huu unapaswa kuwa wa kumsifu Mungu na kuhimizana. Ni wakati wa kuomba na kujifunza mengi juu ya kutii na kumtumika Mungu. Makundi mengi yanafurahia kuimba kabla ya kuanza kujifunza na kuomba. Mwe na wakati wa kushukuru na kusema mambo ya kuombea. Rudieni **Kifungu cha Kukumbuka** wakati mnapokutana ili kusaidia kundi lenu kujifunza vifungu hivi.

Jifunze kila somo kabla ya kukutana. Ni vizuri kwa kila mshiriki wa kundi hili kuwa na nakala ya kitabu hiki. Kiongozi wa mpango anapaswa kusoma na kueleza sehemu ya kwanza na ya mwisho ya kila somo. Waulize watu tofauti wa kundi lenu kusoma na kueleza sehemu zingine. Waambie wengine wasome vifungu vya Biblia vilivyo katika somo hilo.

Vifungu vya kitabu hiki vimetolewa katika Biblia Habari Njema. Tumetumiwa pia Biblia Union Version (UV).

Kila somo linaanza na **Maandiko ya Biblia**. Vifungu hivi vinapaswa kusomewa nyumbani, wala si wakati wa kukutana, kukusaidia kuelewa yale ambayo Biblia inafundisha kuhusu somo hilo. Unapaswa kusomea nyuambani **Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili**.

Vitabu vifuatavyo vimetumiwa kama mwongozo wa kitabu hiki: *Mkristo Akitazama Uwakili Wake*, Davis L. Saunders (Nairobi, Baptist Publicatins House, 1987)*

A Responsible Christian (Nairobi: Kenya Baptist Media, 1995)*

Christian Stewardship, Jeannie Wood (Lusaka, Zambia: Baptist Publishing House)



* Vitabu vingine vya *Iwe Nuru*, pia vitabu vingine tofauti na vifaa na vitabu hivi viwili, vinawezwa kuagizwa kutoka Kenya Baptist Media, P.O. Box 30370, Nairobi, Kenya.

Somo la Kwanza

Vitu Vyote Ni Vya Mungu

Maandiko ya Biblia: Mwanzo 1:1-2:3

Kifungu cha Kukumbuka: *“Dunia na vyote vilivyomo ni vyake Mwenyezi-Mungu; ulimwengu na wote waishio humo ni mali yake.”*

Zaburi 24:1

Sara alisikia sauti za watoto wake, Mariamu na Martha, waliporudi kutoka shuleni. Akawaza, “Je, kwa nini watoto wangu huwa wanabishana kila wakati?” Walipoingia ndani ya nyumba, Sara alianza kuwakosoa.

“Mama, sisi hatubishani,” Mariamu akasema. “Tunajitayarisha kwa ajili ya mchezo wa kuigiza tutakaofanya kanisani. Maneno haya yalisemwa na Mungu! Hebu yasikilize, ‘Wanyama wote porini ni mali yangu, na maelfu ya wanyama milimani ni wangu.’”

Martha alijibu, “Ndege wote wa mwitu ni mali yangu, na viumbe vyote hai mashambani ni vyangu. Fedha na dhahabu yote duniani ni mali yangu.”

Mariamu akamwambia mama yake, “Mchezo wetu unahusu Mungu anavyomilki vitu vyote na utoaji wa zaka.”

Martha akamsahihisha kwa haraka dada yake, “Umekosea. Mchezo wetu unahusu vipawa na karama zote ambazo Mungu hutupatia na jinsi tunavyopaswa kuzitunza.”

Sara alicheka wakati binti zake walipoanza kubishana kuhusu mchezo wao badala ya kufanya mazoezi. Wote wawili walikuwa wakisema ukweli. Mchezo wao ulihusu uwakili. Lakini wao kama watu wengine, hawakuwa maana ya kuwa wakili wa Kikristo. Utajifunza katika kitabu hiki jinsi ya kuwa wakili mwema wa vitu vyote ambavyo Mungu ametupatia.

“Vyote ni Vyangu”

Ni lazima tukubali kwamba vyote vimetoka kwa Mungu ndipo tuweze kuelewa uwakili wa Kikristo. Mungu hakuwa akijisifu wakati aliposema maneno ambayo watoto walirudia kutoka katika Zaburi 50:10-11 na Hagai 2:8. Alikuwa akisema ukweli. Wanyama wote wa porini ni wake na makundu yote juu ya milima elfu ni wa Mungu. Ndege wote wa milimani na wanyama wote mashambani ni wa Mungu. Fedha na dhahabu zote ni za Mungu.

Je, ni nini kinachomfanya Mungu aseme vitu vyote ulimenguni ni vyake? Ana haki kwa sababu ndiye aliyeumba ulimwengu huu na vyote vilivyomo. Hebu tusome Mwanzo 1:1-25.

Mungu aliumba pia mimi na wewe. Alituumba kwa mfano wake mwenyewe. Alituumba tuwe kama yeye. Alituumba ili tutunze ulimwengu wake. Hebu tusome maneno yake katika Mwanzo 1:26-2:3.

“Hapo Mwanzo”

Hebu kwanza tuchukue muda kuangalia tena kifungu cha kwanza katika Biblia zetu. (Mwambie mmoja wao asome tena Mwanzo 1:1.) Maneno ya kwanza katika Biblia yetu ni “Hapo mwanzo.” Mungu alikuwepo kabla ya kuanza kwa ulimwengu. Mungu alikuwepo kabla ya kuanza kwa kitu cho chote ambaco tunaona kila siku.

Musa, katika Zaburi 90:2 anasema, “Kabla kuwapo milima, kabla hujauumba ulimwengu; wewe ndiwe Mungu, milele na milele.” Zaburi 102:25 inasema, “Wewe uliiumba dunia zamani za kale, nbingu ni kazi ya mikono yako.”

Hebu tusome yale ambayo Mungu alimwambia nabii Isaya kuhusu uumbaji wake. (Soma Isaya 44:24 na 45:12.) Je, umewahi kumfikiria Mungu akiumba ulimwengu? Je, unaweza kumwona Mungu akitumia mikono yake kuumba ulimwengu kwa uangalifu? Je, unaweza kumwona akizipanua mbingu?

“Jina Lako Linavyotukuka Duniani Kote!”

Mfalme Daudi alikuwa na kipawa cha kuandika nyimbo nzuri. Zaburi 8 ni wimbo alioandika kumsifu Mungu, mwumba. Daudi alikuwa mfalme tajiri sana na mtumishi aliye chaguliwa na Mungu, lakini alishangazwa na nafasi ya mwanadamu katika uumbaji wa Mungu. Daudi alishangazwa kwamba Mungu alimwona kuwa anastahili kutawala vyote alivyoumba. Hebu tusome Zaburi 8.

Mungu hatuulizi kama tunaelewa jinsi alikuwepo kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu. Wala, hatuulizi tuelewe jinsi alivyopanga na kuumba ulimwengu. Lakini anatutaka tuwe na wajibu kwa vitu alivyoumba.

Wajibu Wetu

Kifungu cha Kukumbuka cha leo kinasema, “Dunia na vyote vilivyomo ni vyake Mwenyezi-Mungu; ulimwengu na wote waishio humo ni mali yake” (Zaburi 24:1). Ni lazima tukumbuke kwamba ulimwengu ni mali ya Mungu. Tunapaswa kutumia vyote tulivyonavyo kwa sababu ameturuhusu kuvitumia. Mwanamke mmoja

alisema hivi, “Ingawa Mungu aliumba na anamilki vitu vyote, na anaweza kufanya kila kitu, aliamua kutenda kupitia kwa mwanadamu kila wakati. Mungu huwapa watu vipawa na karama ili kuutunza ulimwengu.”

Je, utamrusu mtu aishi katika nyumba yako ikiwa haitunzi vizuri? Je, utamwazima jirani yako sahani na vikombe ikiwa hutamtarajia kuvitunza? Tunao wajibu kwa Mungu jinsi tunavyotumia vitu alivyotupatia. Paulo anatumkumbusha juu ya jambo hili katika Warumi 14:12. (Soma kifungu hiki.)

“Kila Kipaji Chema”

Watu wengi hufurahi sana wanapopata zawadi, hasa zawadi wanayotaka au wanayohitaji sana. Yakobo 1:17 inasema, “Kila kipaji chema na kila zawadi kamilifu hutoka mbinguni; hutoka kwa Baba, Muumba.”

Je, umewahi kujisikia kwamba jamaa au marafiki zako hawatambui yale unayowafanyia? Je, unafikiri kwamba wanataka uwafanyie mambo ambayo hupaswi kufanya? Je, huwa unatamani yale ambayo watoto wako au rafiki zako watakwambia, kama, “Asante kwa kunifanyia hivyo.” Je, unafikiri kwamba Mungu huwa anajisikia hivyo wakati mwingine?

Tunapojifunza kitabu hiki cha uwakili, ni lazima tukumbuke kwamba Mungu alitupa yote tuliyohitaji kwa kuishi maisha mazuri. Alitupatia zawadi hizi zote, lakini ametupatia pia zawadi ya kuchagua. Tunaweza kuchagua kutumia zawadi za Mungu kwa njia nzuri. Tunaweza kuchagua kutotumia zawadi hizo au tunaweza kuchagua kutumia kwa njia isiyo faa.

“Mungu Aliupenda Ulimwengu”

Mwanzo 1:31 inasema, “Mungu akaona kila kitu alichofanya kuwa ni chema kabisa.” Mungu hawezi kupendezwa na jinsi sisi na watu wengine walioumbwa wanavyotenda. Lakini, anatupenda sana kiasi kwamba hajatupatia tu zawadi ya uhai hapa duniani. Anatupataia pia zawadi ya uzima wa milele. (Mwambia mmoja wao aseme au asome Yohana 3:16.)

Watu wengi wamepanga mambo ya kufanya na hutumia vizuri wakati wao. Kunao wengine ambao hutumia vizuri mali zao na huwasaidia maskini. Kunao wale wanaofanya kazi kwa bidii kuwatunza wanyama, miti na vitu vingine vilivyoumbwa na Mungu. Watu hawa ni mawakili wazuri, lakini si wote ambao ni Wakristo.

Kitabu hiki ni cha Wakristo ambao wanataka kuwa mawakili wema kwa sababu wanampenda Mungu, mawumba wao. Kitabu hiki ni kwa ajili ya wale wanaotaka kujifunza njia zaidi za kumtumikia na kumtii Mungu. Ni kwa ajili ya Wakristo wanaotaka kujifunza yale ambayo Mungu anatarajia kutoka kwa wale wanaokubali zawadi zake, hasa zawadi ya uzima wa milele.

Tutajifunza katika somo hili jinsi tunavyoweza kumshukuru Mungu kwa yote ambayo ametupatia. Tutajifunza kumsifu jinsi Paulo alivyosema kwamba, “Kwa maana vitu vyote vyatoka kwake, vyote vipo kwa uwezo wake na kwa ajili yake. Utukufu na uwe kwake hata milele! Amina.” (Warumi 11:36).

Kiongozi: Kabla ya kuendelea na mafunzo yetu kuhusu uwakili, ni lazima tujibu maswali yafuatayo. Hebu tuinamishe vichwa vyetu na tufunge macho yetu. Jibu kila mojawapo ya maswali haya kimoyomoyo.

- ❖ Je, nimepokea zawadi ya Mungu ya uzima wa milele? Je, ninauhakika kwamba ameniokoa? Ikiwa jibu lako kwa maswali yote mawili ni la, utapaswa kusoma kwa makini “Mpango wa Mungu wa Wokovu” ulio sehemu ya mwisho ya kitabu hiki. Zungumza na mchungaji wako au rafiki Mkristo kabla ya mkutano wetu ujao. Waulize wakusaidie kuelewa jinsi unavyoweza kupata zawadi ya Mungu ya uzima wa milele.
- ❖ Je, ninamkubali Mungu kuwa mwenye milki za vitu vyote, mimi na mali yangu? Je, ninataka kuwa mtumishi wake na kumtii kila wakati?
- ❖ Je, niko tayari kumruhusu Mungu anifundishe jinsi ya kuwa wakili mwema. Je, niko tayari kuwa wakili mwema wa zawadi na karama zote alizonipatia Mungu?

Hebu tufunge kwa kusoma Zaburi 100 na tuitumie wakati inapotuongoza kwa kufunga kwa maombi. Unapoomba, mwambie Mungu kwamba *unamwabudu kwa furaha*. Mwombe akuongoze unapokubali kwamba *yeye ni Mungu wetu na ndiye aliye tuumba*. Mwombe akusaidie kuwa shahidi imara na kuuonyesha ulimwengu kwamba sisi ni kondoo wake. Omba kwamba tutaweza kuwaambia wengine kwa ujasiri kwamba *“Mwenyezi-Mungu ni mwema; fadhili zake zadumu milele, na uaminifu wake katika vizazi vyote.”*



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Isaya 45:1-8
Siku ya 2) Isaya 45:9-19; Siku ya 3) Zaburi 103:1-14;
Siku ya 4) Zaburi 104:1-9; Siku ya 5) Zaburi 104:10-18;
Siku ya 6) Zaburi 104:19-26; Siku ya 7) Zaburi 104:27-35

Wakili Mwema na Mwaminifu

Maandiko ya Biblia: Mathayo 25:14-30

Kifungu cha Kukumbuka: *"Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu. Hapo tena inayohitajiwa katika mawakili, ndiyo mtu aonekane kuwa mwaminifu."* (1 Wakorintho 4:1-2, UV)

Mariamumu alikuwa ameahidi kwa miaka mingi kwamba atamtembelea mwanawe kule Marekani. Mashamba yake yote yalikuwa yanaendelea vizuri na alikuwa amepata faida nyingi mwaka ulopita. Ulikuwa wakati mzuri wa kwenda kumtembelea.

Mariamumu aliwaita nyumbani kwake wafanya kazi wake watatu. Akamwambia Tom awe akichunga shamba lake kubwa la mboga. Edith, mkewe Tom, aliambiwa asimamie shamba la mifugo. Joel alipewa usimamizi wa shamba ndogo la maua. Mariamumu alimwambia kila mmoja afanye uamuzi wa wote unaohusu shamba alilopewa na faida yake wakati wa safari yake.

Mariamumu alirudi nyumbani baada ya mwaka mmoja, akawaita tena nyumbani kwake Tom, Edith na Joel. Tom na Edith walimwambia kwamba wao walikuwa wamehudhuria masomo ya ziada. Walikuwa wamejifunza njia na ujuzi mpya wa kutumia shambani. Walinunua mbolea mpya ya kuweka shambani pa kupanda na kwa malisho ya ng'ombe. Waliwaajiri mafundi wa kujenga mitambo ambayo ilikuwa imeharibika. Mambo haya na mengine mengi yaliongezea faida yao.

Walimpatia Mariamumu makaratasi ya kuonyesha gharama na faida walizopata kutoka kwa mashamba waliyosimamia. Wakamwambia kwamba shamba alilotaka kununua lililo karibu na lile la mifugo, sasa linauzwa. Walikuwa tayari wamepanga anunue kwa kutumia faida waliyopata wakati alipokuwa safarini.

Joel alimwambia Mariamumu shida na matatizo ya kila aina kuhusu shamba la maua. Ugonjwa ulikuwa umeharibu maua mengi. Gari walilotumia kupeleka maua sokoni lilikuwa limeharibika. Akamwambia, "Niliogopa kwamba nitatumia pesa zako nyingi. Dawa ya ugonjwa huo ilikuwa ya bei ghali, kwa hivyo sikuinunua. Ingenigharimu maelfu ya pesa kutengeneza gari hilo. Niliona ni afadhali uamue wewe mwenyewe ikiwa tutatengeneza gari hilo. Hizi ndizo pesa zote ulizonipatia. Nilizifungua vizuri katika sanduku langu."

Mariamamu akamwambia Joel, “Wewe mfanya kazi mvivu. Ungeweka pesa zangu katika benki. Ningepata faida ndogo kutoka benki. Kuanzia leo, wewe si msimamizi wa shamba la maua!”

Akawaambia Tom na Edith, “Vyema, watumwa wema na waaminifu! Mmekuwa waaminifu kusimamia mashamba madogo, sasa nitawafanya msimamie mashamba makumbwa. Ingieni mfurahi pamoja nami. Mtaendelea kusimamia shamba langu la mboga na ng’ombe. Tom, sasa utasimamia pia lile shamba langu jipya. Nawe Edith, nataka usimamie pia shamba la maua.”

Hadithi iliyo hapo juu si ya kweli, lakini ni hadithi ambayo inaweza kutendeka. Ni hadithi ambayo inakusaidia kuelewa maana ya kuwa wakili Mkristo.

Mfano wa Watumwa Watatu

Yesu alitumia mifano kuwasaidia wafuasi wake kuelewa maana ya ukweli wa kiroho aliokuwa akifundisha. Hebu tusome mfano ulio katika Mathayo 25:14-30. (Mwambie mmoja wao au kadhaa wasome vifungu hivi.)

Katika *Mfululizo wa Kusoma Biblia Kila Siku*, William Barkley anasema kwamba Yesu alikuwa akifundisha mambo yafuatayo katika mfano huu:

- 1) Mungu hutupatia vipawa na karama tofauti, lakini anatutarajia tuwe na wajibu kwa kila karama au kipawa tulichopewa. Anatutarajia kila mmoja atumie kile aliche nacho vizuri kumfanyia kazi.
- 2) Tuzo ya kazi nzuri iliyofanywa ni kupewa kazi nyingine nyingi. Watumwa waaminifu walipewa kazi muhimu zaidi za kufanya.
- 3) Mtumishi mvivu hakuadhibiwa kwa kupoteza pesa au kutumia pesa nyingi. Aliadhibiwa kwa kutofanya cho chote.
- 4) Mtu anapotumia uwezo wake, huweza kutumia zaidi karama hizo kwa ajili ya Mungu na wengine. Mtu ambaye hawzi kutumia uwezo wake, hupoteza uwezo huo.

“Aliwaita Watumishi Wake, Akawakabidhi Mali Yake”

Hebu tusome Mwanzo 1:26 na Mathayo 25:14 na ujibu maswali yafuatayo:

- ❖ Je, nchi, wanyama na mimea ni mali yetu?
- ❖ Je, zile talanta au pesa watumwa walipewa katika Mathayo 25 zilikuwa zao?

❖ Je, mashamba ya Mariamu yalikuwa mali ya watu aliochagua kusimamia?

Majibu yetu kwa maswali haya ni sehemu ya maelezo ya uwakili wa Kikristo. *Wakili ni mtu ambaye anatanza mali ambayo ni ya mtu mwingine.* Watumwa walio katika Mathayo 25 hawakupewa umilkaji wa mali ya mwenyewe. Kama Mariamu katika hadithi yetu, aliwauliza watu kutunza mali yake wakati alipokuwa hayupo.

Tulikumbushwa katika somo letu lililopita kwamba kila kitu tulicho nacho hutoka kwa Mungu. Mungu hutupatia zawadi ya uzima na kila kitu tunachohitaji kuishi hapa duniani. Tasisahau kwamba Mungu anatarajia tutunze ulimwengu wake na vyote alivyotupatia.

“Umekuwa Mwaminifu”

Hebu tusome Mwanzo 1:27-28 na Mathayo 25:21, 26-27 na kifungu cha pili cha kukumbuka, 1 Wakorintho 4:2. Watumwa watatu na watumishi wa Mariamu waliweza kurudisha kile ambacho walikuwa wamepatiwa. Wote walikuwa na wajibu wa kutunza kile walichopewa. Je, watumishi wema walifanya nini tofauti kutoka kwa watumishi wabaya? (Wape muda wa kujibu)

Wakili anatarajiwa kuwa msimamizi mwema. Anatarajiwa kufanya zaidi ya kuweka vizuri mali anayopewa. Ni lazima atunze mali hiyo kama kwamba ni yake. Ni lazima ailinde na kuitumia vizuri. Ni lazima aisaidie kukua na kuikuza.

“Akaja Bwana, Akafanya Hesabu Nao”

Hebu tusome Mathayo 25:19 na Warumi 14:12 na tujibu maswali yafuatayo:

- ❖ Je, Mariamu aliye katika hadithi yetu na yule mtu katika mfano wa Yesu walikuwa na haki ya kuuliza hesabu ya mali yao?
- ❖ Je, walikuwa na haki kutarajia mawakili wao kuwa wametunza mali zao?
- ❖ Je, Mungu ana haki ya kutupa wajibu wa kutunza vipawa na karama alizotupatia?

Wakili mwema anajua kwamba anatanza mali ya yule mtu mwingine. Mwenye mali atataka hesabu au ripoti ya jinsi alivyotunza mali yake. Kwa hivyo, wakili ni mtu ambaye anatanza na anaowajibu kwa mali aliyopewa na mtu mwingine.

“Vema, Mtumishi Mwema na Mwaminifu”

Je, ni nini maana ya wakili Mkristo mwema na mwaminifu? *Mawakili Wakristo wema na waaminifu ni wanaume na wanawake ambao wanajaribu kuwa wasimaminzi wema wa vipawa na karama walizopata kutoka kwa Mungu. Wanatarajia na wako tayari kumruhusu Mungu kuwahukumu jinsi wanavyotunza karama hizo.*

Wakristo wanaweza kuwa kama mtumwa aliyeficha mali aliyopewa, wala hakufanyia cho chote. Tunaweza kuamua kutumia au kukuza karama tunazopewa na Mungu. Bwana Barclay, katika mafunzo yake, anasema kwamba karama na zawadi zitokazo kwa Mungu hazitoshani, lakini Mungu anatarajia juhudi zetu kutoshana. Mungu anamtarajia kila mtu kutumia kwa ukamilifu uweza alionao.

Katika mfano wa Yesu wa “Watumwa Watatu” anafundisha kwamba Mungu hatatuadhibu kwa kutotumia karama alizotupatia. Atatuadhibu ikiwa hatutakubali kwamba yeye ndiye mwenye mali yote tuliyo nayo.

Kiongozi: Sehemu nyingine ya maelezo ya wakili ni mtu ambaye anaweza kuaminiwa. Mungu huwaamini wanaume na wanawake kwamba watatunza vitu alivyoumba. Kila mmoja wetu anaweza kusema, “Mungu ananiamini kutunza vitu vyote alivyoumba!” Hebu tusome Zaburi 8:3-8 na Kifingu cha Kukumbuka cha leo, 1 Wakorintho 4:1-2.

Hebu tuombe kwamba tunaposoma kitabu hiki, tutakua katika hali yetu na uwezo wa kuwa mawakili wema na waaminifu wa karama na vipawa ambavyo Mungu ametupatia. Hebu tuombe kwamba Mungu, mwumba wetu na mwenye mali yote, atatupata tukiwa tunastahili uaminifu wake.



Vifungu vya Biblia vyo Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Zaburi 24; Siku ya 2) 1 Mambo ya Nyakati 29:10-17; Siku ya 3) Nehemia 9:1-8; Siku ya 4) Nehemia 9:9-18; Siku ya 5) Nehemia 9:19-25; Siku ya 6) Nehemia 9:26-31; Siku ya 7) Nehemia 9:32-38

Biblia Yetu na Uwakili

Maandiko ya Biblia: Mathayo 5:17-20

Kifungu cha Kukumbuka: *"Majani hunyauka na ua hufifia; lakini neno la Mungu wetu ladumu milele."* Isaya 40:8

Hivi maajuzi gazeti la East African lilisimulia hadithi ya ajali ya barabarani ambayo ilifanyika karibu na hospitali. Mtu mmoja katika ajali hiyo alikuwa anakufa. Msamaria mwema alienda katika hospitali hiyo na kuwaomba msaada. Alishangaa wakati madakari wala wauguzi wa hospitali hiyo walipokataa kwenda naye. Wakamjibu, "Hii ni hospitali ya watoto. Hatuwatibu watu wazima."

Mtu yule aliyejeruhiwa alikufia hapo. Jamaa yake watakuwa wakijiuliza kila mara kama angepona ikiwa madaktari hao wangemsaidia. Bila shaka, madaktari na wauguzi hao watakuwa wakijiuliza kila wakati, kama kweli walitii sheria na maagano ya hospitali yao.

Tunapoishi hapa duniani tunafundishwa kwamba sheria zinahitajika kutuongoza na kutulinda. Watoto wanapoanza kutembea hufundishwa kutogusa vitu fulani au kutoenda mahali fulani. Hali, mzazi hawezi kumpa mtoto wake kila sheria ambayo itamfanya asiumei.

Ni lazima tujifunze kutumia sheria kutuongoza na kutusaidia kufanya uamuzi wa busara. *Ni lazima tujifunze pia kwamba utiifu ni zaidi ya kutii tu sheria. Utiifu halisi huhitaji hali ya kuelewa sababu ya kuwepo sheria.* Yesu alipokuwa hapa duniani aliwasaidia wafuasi wake kuelwa jinsi ya kutii sheria za Mungu.

Amri za Sheria

Watu wengi wa wakati wa Yesu walimwogopa sana Mungu. Wayahudi walijifunza na kujaribu kutii amri na sheria zote zilizo katika Agano la Kale jinsi mababu zao walivyofanya. Saulo, ambaye aliitwa baadaye Paulo, alikuwa mfano mzuri wa watu hawa. Katika Wafilipi 3:6, anasema kwamba, "Kuhusu uadilifu unaopatikana kwa kuitii sheria, mimi nilikuwa bila hatia yoyote." Hebu tusome jinsi Paulo anavyoelezea hamu yake ya kumtii Mungu na sheria zake katika Matendo 22:3-5.

Paulo, kama viongozi wengine wa kidini wa siku zake, alijua kutoka kwa masomo yake kwamba Mungu alikuwa ameahidi

kumtuma Mwokozi na mfalme. Wengi wa viongozi hawa hawakuamini kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu aliyeahidiwa. Hawakuelewa kwa nini Yesu alikuja duniani.

Yesu alielewa hali ya viongozi hawa. Je, unakumbuka “Mfano wa Watumwa Watatu” ambao tulijifunza katika somo la kwanza? Katika *Mfululizo wa Kusoma Biblia Kila Siku*, William Barclay anasema kwamba Yesu alikuwa akifundisha wanafunzi wake kwamba viongozi wa kidini wa siku hizo walikuwa kama watumwa waovu.

Watu hawa waliogopa mabadiliko ya kufanya mambo kwa njia mpya. Walipenda kuwa na sheria za Agano la Kale kama mwongozo wao. Walitosheka kujua na kuhusiana na Mungu kupitia kwa sheria na amri hizi. Sheria na amri hizi ndizo zile mababu zao walifuata na kuwafundisha watoto wao kwa maelfu ya miaka.

Agano la Kale na Agano Jipya

Biblia yetu imegawanywa katika sehemu mbili, Agano la Kale na Agano Jipya. Neno Agano linamaana ya mapatano au uhusiano. Agano la Kale linazungumzia kuhusu mapatano au uhusiano kati ya Mungu na wanaume na wanawake miaka mingi kabla ya kumtuma Yesu duniani. Sheria na amri zile nyingi ambazo Mungu alimpatia Musa na wengine ili watu wake watii zinapatikana katika sehemu hii ya Biblia.

Agano Jipya linazungumzia kuhusu mapatano au uhusiano mpya kati ya wanaume na wanawake na Mungu kupitia kwa Yesu. Yesu alipokuwa hapa duniani alianza kuwaambia kuhusu mapatano au uhusiano huu mpya. Hebu tusome vifungu vifuatavyo na tukamilishe sentenzi zifuatazo kuhusu Yesu.

❖ *Yohana 3:16* “Maana Mungu aliupeneda _____ hivi hata akamtoa Mwana wake wa pekee, ili kila amwaminmiye asipotee, bali awe na uhai wa milele.”

❖ *Yohana 14:6* “Yesu akamjibu, “Mimi ni _____, na _____, na _____. Hakuna awezaye kwenda kwa _____ ila kwa kupitia kwangu.”

❖ *Yohana 14:26* “Msaidizi, _____, ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, atawafundisha kila kitu na kuwakumbusheni yote niliyowaambieni.”

Je, kulifanyika nini kilichomfanya Paulo aelewe uhusiano mpya ambao Yesu alikuwa ameelezea? Alikutana na Yesu! Hebu tusome ushuhuda aliomtolea mfalme katika Matendo 26:9-18.

Paulo alitambua kwamba Yesu alikuwa Masihi ambaye aliahidiwa na waandishi wa Agano la Kale. Paulo alijifunza kwamba hangepokea wokovu wa Mungu kwa kutii sheria. Mungu alikuwa akipeana uzima wa milele kwa wale walioamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na kumpokea kuwa Bwana na Mwokozi. Mwanadamu angekuwa na uhusiano mpya na Mungu kupitia kwa Yesu. Hebu tusome jinsi Paulo alivyoelezea Wakristo wa Rumi kuhusu jambo hili katika Warumi 3:21-26.

Amri Kuu Katika Sheria

Viongozi wa kidini walimwuliza Yesu maswali mara kwa mara ili kumshika na kuthibitisha kwamba hajatoka kwa Mungu. Mathayo 22:34-38 inatuambia mojawapo ya wakati kama huu. Soma vifungu hivi na ukamilishe sentenzi zifuatazo ambazo ni jibu la Yesu. “Mpende _____ wako kwa _____ wako wote, na kwa _____ yako yote na kwa _____ yako yote.”

Viongozi wa kidini hawakufanikiwa kumjaribu Yesu. Yesu aliwaambia kwamba walipaswa kutii sheria zao za kale, lakini walipaswa kuzitii kama watu waliokuwa na uhusiano mpya na Mungu. Hawakupaswa kumtii Mungu kama watu ambao walihofia kuadhibiwa. Walipaswa kutii sheria za Mungu na kumtumikia kwa sababu walimpenda.

Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na alijua jinsi ya kujibu maswali yote ambayo aliulizwa akiwa hapa duniani. Alijua mpango wa Mungu kwa wanaume na wanawake chini ya uhusiano mpya na Mungu. Alielewa kwamba sheria za Mungu ambazo zimeandikwa katika Agano la Kale zilihitajika na hazikupaswa kusahaulika. Hebu tusome yale aliyowaambia wafuasi wake katika Mathayo 5:17-20.

“Nimekuja . . . Kukamalisha”

Uelewaji wetu kuhusu uhusiano wetu wa kale na uhusiano mpya ni sehemu ya kile kinachotufanya tuwe tofauti kama Wabatisti. Siku hizi, kuna watu wa dini zingine ambao wanaamini kwamba watu wanastahili kutii tu sheria na amri za Agano la Kale. Wengine wanaamini kwamba wafuasi wa Kristo wanapaswa kutumia tu sheria na amri za Agano Jipya kama mwongozo wao.

Sisi kama Wabatisti tunaamini kwamba Roho wa Mungu aliwaongoza waandishi wa Agano la Kale na Agano Jipya. Hasa hutaka kuelewa Biblia yote kama Wakristo. Jambo hili hutufanya tusome na tuelewe Agano la Kale katika njia tofauti kuliko wale watu ambao walisoma mara ya kwanza. Tunajua kwamba Yesu alikuwa akisema ukweli wakati aliposema, “Msidhani kuwa nimekuja kutangua sheria na mafundisho ya manabii. Sikuja kutangua bali

kukamilisha.” (Mathayo 5:17). Tunajua kwamba Yesu ndiye utimilifu wa Agano la Kale.

Tunasoma Biblia yote kama watu ambao wamepata nafasi ya kukubali upendo na wokovu wa Mungu kupitia kwa Mwanawe, Yesu Kristo. Sisi si watu ambao tuliishi kabla ya Yesu kuja hapa duniani. Tunaishi chini ya agano na uhusiano mpya na Mungu, wala si lile Agano la Kale. Tuna mfano wa Yesu wa kufuata na Roho Mtakatifu aliye ndani yetu, hutufundisha na kutuongoza. Hebu tusome Waebrania 1:1-3 na maneno ya Yesu katika Yohana 14:14-17.

Tunaamini kwamba mafundisho ya Yesu katika Agano Jipya yanapaswa kuwa mwongozo wetu katika imani na matendo. Hii haifanyi Agano la Kale lisiwe muhimu. Ni lazima tujifunze Biblia yetu yote ikiwa tunataka kujua na kuelewa Mungu wetu na mipango yake kwa watu wake.

Kiongozi: Je, kwa nini tunapaswa kujifunza Agano la Kale na Agano Jipya kama kitabu kuhusu uwakili? Tukijifunza Biblia yote tutajua sababu ya kutaka kuwa wakili. Jiulize maswali haya: *Je, unafuata sheria na amri kuhusu uwakili kwa hofu ya kuadhibiwa na Mungu au kwa sababu unamtii Mungu? Au wewe ni wakili mwema kwa sababu unampenda Mungu kwa moyo wako wote, na roho, na akili zote? Je, upendo huu unakufanya utake kumtii Mungu na kumtumikia?*

Ni lazima tutambue pia kwamba yote tunayofanya ni sehemu yetu ya kushuhudia kama Wakristo. Watu wengine huona jinsi tunavyotumia wakati wetu, pesa, mali na ufahamu wa Mungu. Matendo yetu yanawaonyesha uhusiano wetu na Mungu. Tutajifunza jambo hili katika somo linalofuata.

Hebu tusome maneno ya Mungu kwa nabii katika Yeremia 31:31-34. Ni lazima tujue kuhusu mapatano na uhusiano wa Agano la Kale na Agano Jipya ili tuelewe jinsi ya kutumia sheria na amri zilizo katika Agano la Kale. Tunaweza kuwa kama viongozi wa kidini wa wakati wa Yesu na kuzifuata tu kama sheria. Au tunaweza kuzitumia kama mwongozo wa mioyo yetu tunapotafuta kumtumikia na kumtii Mungu. *Hebu tuombe kwamba tutakuwa mawakili wema Wakristo kwa sababu tunampenda Mungu kwa moyo, roho na akili zako zote.*



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Matendo 24; Siku ya 2) Matendo 25; Siku ya 3) Waebrania 8:1-6; Siku ya 4) Waebrania 8:7-13; Siku ya 5) Waebrania 9:1-14; Siku ya 6) Waebrania 9:15-28; Siku ya 7) Luka 22:14-23

Uwakili wa Maisha Yangu

Maandiko ya Biblia: Warumi 11:33-12:2; Yakobo 2:14-26

Kifungu cha Kukumbuka: *"Kwa hiyo, ndugu zangu, maadamu Mungu ni mwenye huruma nyingi, nawashihi kwa moyo wote: jitoleeni nafsi zenu kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai, takatifu na yenye kumpendeza. Hii ndiyo njia yenu halisi ya kumwabudu.."*

Warumi 12:1

Evelyn alisikia mlango ukibishwa wakati alipokuwa anachukua Biblia yake na kitabu cha *Iwe Nuru* tayari kwenda kanisani. Alifikiria kutokea mlango wa nyuma, lakini akaamua kuona yule aliyekuwa akibisha mlango. Alishika funguo na vitabu vyake mkononi kuonyesha kwamba anatoka.

Pale mlangoni alikutana na mama mmoja mwenye watoto watatu. Mgeni huyo alimwelezea kwamba yeye na watoto wake walikuwa wametoka nyumbani kwao kwa sababu ya mafuriko. Hawakuwa na mahali pa kukaa, chakula wala pesa. Alikuwa ameambiwa kwamba Evelyn ni Mkristo na anaweza kumsaidia.

Evelyn akafikiria, "Mimi ndiye ninaongoza leo. Wanawake wananingojea. Nina pesa kidogo na kijitabu cha injili katika Biblia yangu ambacho ninaweza kumpatia. Nitamwambia pia kwamba nitauliza kanisa langu wamwombee yeye na jamaa yake. Kisha nitamwambia aende."

Ikiwa tutaachia hadithi hii mahali hapa, inaweza kuwa mfano wa kufundishia katika Yakobo 2:14-16. Tunaposoma vifungu hivi, jiulize swali hili? Je, umewahi kumtendea mtu jinsi hiyo?

Msaidizi Wetu, Roho wa Mungu

Haikuwa kosa kwa Evelyn kumpatia mama yule pesa, kijitabu cha injili na kuahidi kumwombea. Angefanya zaidi ya hayo. Je, Evelyn au Mkristo anawezaje kujua wakati na kiwango cha kusaidia wengine? Tunaweza kujua jinsi na wakati wa kumtumikia Mungu kwa kutegemea uhusiani wetu naye kama Wakristo. Ni lazima tutegemee Roho Mtakatifu ambaye yuko ndani yetu. Hebu tusome Yohana 14:16-17.

Hebu tufikirie jinsi nyingine ya kumalizia hadithi yetu. Evelyn angeopa apate msaada. Angumwuliza Mungu amwonyeshe jinsi ya kuweza kumsaidia mama yule. Evelyn angemwalika mama yule kuhudhuria ushirika wa wanawake kanisani mwake. Angewaambia

wanawake wa ushirika wake kumsaidia kutafuta mapenzi ya Mungu kutimiza mahitaji ya mgeni yule.

“Nitakuonyesha Imani Yangu”

Wakristo wengi wanataka tu Mungu awatumie kwa njia ndogo ndogo na rahaisi. Wengine huamini kwamba wao ni Wakristo wema wakati wanapotii sheria fulani za Biblia na kufanya mambo kama kuhudhuria kanisa. Yakobo alielewa hivyo wakati alipoandika barua yake kwa “watu wote wa Mungu duniani kote” (Yakobo 1:1).

Yakobo aliandika kwamba Mungu hataki watoto wake kujua tu Neno lake na kuwa wema na wenye haki. Mungu anahitaji matendo yetu yaongozwe na uhusiano wetu naye kila wakati na kila siku ya maisha yetu. Maisha yetu ndiyo ushuhuda wetu mkuu au njia ya kuwaambia wengine juu ya upendo na wokovu wa Mungu. (Soma Yakobo 2:18-24).

Haitakuw arahisi kumtumikia Mungu kila wakati na kila siku. Lakini tutataka kumtumikia na kumtii Mungu ikiwa tunampenda kwa moyo wetu wote, roho na akili. Pia, tutataka kutumia vizuri karama nyingi ambazo Mungu ametupatia wakati tunapomtumikia na kumtii.

Haya ndiyo maelezo kamili ya uwakili wa Kikristo. Uwakili wa Kikristo siyo kufanya mambo mema na kufuata sheria. *Uwakili kamili ni kumruhusu Mungu akutumie sisi na vyote tulivyo navyo kumtumikia na kumtii.*

Uwakili wa Kikristo Ni Sehemu ya Ushuhuda Wetu

Huwa tunazungumzia kuhusu ushuhuda wa Mkristo. Ni lazima tuwe tayari kila wakati kuwaambia wengine mpango wa Mungu wa wokovu. Lakini, ushuhuda wetu wa Kikristo ni zaidi ya jinsi tulivyojipangia wakati wa kuwaambia wengine juu ya upendo na wokovu wa Mungu. Huwa tunashuhudia au kuwaambia wengine juu ya uhusiano wetu na Kristo katika maisha yetu ya kila siku. Jinsi tunavyotenda na kufanya huwaonyesha wengine yale tunayoamini kuhusu Mungu na jinsi alivyo wa muhimu kwetu.

Uwakili wa karama ambazo Mungu ametupatia ni sehemu muhimu ya ushuhuda wetu. Jinsi tunavyotumia wakati wetu, pesa, mali na hekima ya Mungu huwaonyesha watu wengine jinsi Mungu alivyo wa muhimu maishani mwetu. Jinsi tunavyotumia nyumba zetu na kuwatimizia wengine mahitaji yao, huwa sehemu ya ushuhuda wetu. Matendo yetu huwaonyesha wengine jinsi tunavyompenda na kutaka kumtumikia Mungu.

Utajiri wa Mungu

Watu wengi hawataki kujifunza juu ya uwakili wa Kikristo. Hufikiri kwamba mafunzo hayo yatahusu tu pesa na zaka (fungu la kumi). Wakili mwema Mkristo atataka kutoa zaka na sadaka. Mawakili Wakristo wanaompenda Mungu na wanaotaka kumtumikia na kumtii, hujua kwamba wamepokea mengi kutoka kwa Mungu wala sio tu pesa yake. Wanajua kwamba wao ni matajiri wa vitu vingine pia. Paulo, katika barua yake kwa Warumi, anarudia maneno kutoka kwa Agano la Kale ya kumsifu Mungu. Hebu tusome vifungu hivi, Warumi 11:33-35, ambavyo vinatukumbusha kwamba vyote tulivyo navyo vinatoka kwa Mungu.

Wakati Paulo anapotumia maneno utajiri wa Mungu, Je, anazungumzia kuhusu pesa? La! Paulo anazungumzia kuhusu hekima ya Mungu ambayo ilimfanya amwokoe mwanadamu. Hebu tusome pia Warumi 2:4.

Tutajifunza katika kitabu hiki jinsi ya kuwa wakili mwema wa pesa na mali yako na maana ya kutoa zaka. Tutajifunza pia jinsi ya kuwa wakili mwema wa karama tulizopewa na Mungu. Hebu tuangalie masomo ambayo tutajifunza baadaye katika kitabu hiki. (Fungua katika ukurasa wa Yaliyomo na usome majina ya vichwa vya kuanzia Somo la Tano hadi Kumi na Tatu.)

“Jitoleeni Nafsi Zenu . . . Kama Dhabihu Iliyo Hai”

Hebu tusome pamoja Kifungu cha Kukumbuka cha leo, Warumi 12:1. Watu wengi hujifunza na kukumbuka tu “Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyohai,” yaani sehemu ya katikati ya kifungu hiki. Paulo anaeleza pia katika kifungu hiki sababu ya kuitoa miili yetu kama dhabihu na jinsi ya kufanya hivyo.

Paulo anasema kwamba tunapaswa kuitoa miili yetu iwe dhabihu iliyo hai kwa Mungu “maadamu Mungu ni mwenye _____ nyingi.” Hebu tusome pia Warumi 11:36, kifungu kilicho kabla ya Kifungu cha Kukumbuka cha leo. Ni lazima tukumbuke kwamba vyote tulivyo navyo vimetoka kwa Mungu. Hatustahili vitu hivi, ni zawadi tulizopewa na Mungu wetu mwenye hekima na upendo.

Je, tunawejaze *kuitoa miili yetu iwe dhabihu iliyo hai kwa Mungu*? Paulo anaandika kwamba, “jitoleeni nafsi zenu kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai, takatifu na yenye kupendeza. Hii ndiyo njia

yen halisi ya _____.” Hatuwezi kuwa dhabihu iliyo hai mpaka tuamue kumtumikia Mungu kama Bwana wetu. Ni lazima pia tujitoe kufanya mapenzi yake kila wakati na kila siku, sio tu wakati tuliotenga wa kanisa au tuliopanga kwenda kushuhudia.

Uwakili ni Sehemu ya Kuabudu

Wakristo wanaojitoa kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai watakuwa mawakili wema wa vyote walivyo navyo. Watajua kwamba kuwa Mkristo ni zaidi ya kusoma Biblia na kuhudhuria ibada za kanisa. Kuwa Mkristo ni zaidi ya kuomba na kutoa sadaka. Kuwa Mkristo ni kumpenda Mungu na kutafuta mapenzi yake na kuwa tayari kumtumikia na kumtii.

Wakristo ambao wametoa maisha yao kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai, watataka kutumia hekima, maarifa, ujuzi na vipawa kumtumikia Mungu. Watatamani kuongozwa na Mungu kila wakati. Watamfanya Mungu kuwa msingi wa maisha yao. Watataka kila wakati kumfikiria Mungu. Watakuwa wakitafta mapenzi ya Mungu na kujaribu kumtumikia wakitumia karama na vipawa vyao.

Kiongozi: Maisha ya wakili mwema Mkristo huonyesha wengine kwamba wanampenda Mungu kwa moyo wao wote, roho na akili. Wakili mwema hamwamini tu Mungu na kutaka kumpenda. Wakili mwema hutaka kutumia karama na vipawa vyake kumtumikia na kumtii Mungu.

Juma lijayo tutazungumzia juu ya majibu yenu kwa maswali haya: *Je, mimi ni wakili Mkristo wa aina gani? Je, niko tayari kuutoa mwili wangu kama dhabihu iliyo hai? Je, niko tayari kujitoa mimi na vyote nilivyo navyo kumtumikia na kumtii Mungu kila wakati na kila siku?*

Paulo anatukumbusha uhusiano na wajibu maalum tulionao na Mungu katika 1 Wakorintho 6:19-20. (Soma kifungu hiki.) Hebu tumshukuru Mungu kwa vyote alivyotupatia. Tuombe kwamba tutawaonyesha wengine kwamba yeye anaishi ndani yetu nasi ni watu wake. Hebu tuombe kwamba tunapoendelea kujifunza kitabu hiki, tutajifunza mengi jinsi ya kujitoa kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai.



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Isaya 40:12-24; Siku ya 2) Isaya 40:25-31; Siku ya 3) Warumi 6:1-11; Siku ya 4) Warumi 6:12-23; Siku ya 5) Yakobo 1:19-27; Siku ya 6) Yakobo 2:14-26; Siku ya 7) Yakobo 3:1-12

Wakati na Upendo Wangu kwa Mungu

Maandiko ya Biblia: Zaburi 1; Wakolosai 1:9-14

Kifungu cha Kukumbuka: *"Umtambue Mungu katika kila ufanyalo, naye atazinyosha nija zako."* Mithali 3:6

Sara alienda kanisani baada ya kumtembelea rafiki yake. Alikuwa amechoka lakini alikuwa bado na mengi ya kufanya. Alifurahi alipoambiwa na mchungaji wake kwamba waombe pamoja, lakini ombi lake lilimshangaza sana. "Baba, msaidie Sara afanye uamuzi mzuri jinsi anavyotumia wakati wake. Msaidie ajifunze kukupenda zaidi."

Sara alipokuwa akienda nyumbani, akawaza, "Je, kwa nini aliomba kwamba *nijifunze jinsi ya kumpenda Mungu zaidi!* Mimi hufundisha masomo ya Biblia. Huwa nakutana kila juma na kundi linalojifunza jinsi ya kuwafanya wengine kuwa wanafunzi. Huwa nawatemelea kila siku watu wenye shida. Nina jishughulisha sana na kazi ya Mungu mpaka sipati nafasi ya kumaliza kazi zangu za nyumbani wala kuwa na wakati wa kufanya mambo yangu. Jamaa yangu, majirani na marafiki wana mahitaji mengi sana ambayo Mungu anataka mtu awatimizie."

Sara alimsikia Mungu akuinena naye wakati hasira yake ilipozidi kuongezeka. Alimwuliza swali alilimwuliza Petro katika Yohana 21:15, "Je, wanipenda mimi?"

Sara akalia akisema, "Ee Bwana, wewe wajua kwamba nakupenda. Huwa natumia muda mwingi kila siku nikikutumikia. Hufanya kila mara kazi yako."

Kisha akamsikia Mungu akisema, "Mwanangu, ni vizuri kunifanyia mengi, lakini ninataka nyinyi nyote mwe na wakati mwingi nami."

Je, ina maana gani *kuwa na wakati na Mungu*? Je, upendo wetu kwa Mungu huhusu vipi jinsi tunavyotumia wakati wetu? Je, tunaweza kupata wapi majibu ya maswali haya? Hebu tuangalie mafundisho na mifano ya Neno la Mungu.

"Kama Mtu na Rafiki Yake"

Hebu mfikirie rafiki unayempenda sana. Huwa tunataka kuwafanyia mambo fulani. Pia, hutaka kuwa nao na kujua vizuri. Hutaka pia uhusiano wetu ukue.

Je, huwa unakuza vipi uhusiano wako na marafiki? Hukaa nao kwa muda mrefu. Hutumia muda mrefu kuzungumza nao na kuwasikiliza. Huweza kuwaonyesha kwamba unathamini urafiki wao na yale wanayokufanyia. Huwaonyesha kwamba unawahitaji.

Musa alikuwa na uhusiano maalum na Mungu. Kutoka 33:11 inasema, “Hivyo ndivyo Mwenyezi-Mungu alivyokuwa akiongea na Mose uso kwa uso, kama mtu na rafiki yake.” Mungu anatupenda na anatakua tuwe na uhusiano kama huu naye. Ni lazima tuwe na wakati naye ndipo ifanyike hivyo. Ni lazima tuwe na wakati wa kumjua. Ni lazima tuzungumze naye.

Hebu angalia tena yale tuliyojifunza kuhusu urafiki. Je, unaona maneno, uhusiano na wakati yakitumiwa sana? Ikiwa tunatake kuwa mawakili wema Wakristo wa wakati wetu ni lazima tuwe na uhusiano mwema na Mungu.

“Yatupasa Kuendelea Kufanya Kazi”

Kila mtu ana kiwango tofauti cha wajibu na mali ya kutunza kila siku. Lakini sote tuna jambo moja ambalo ni sawa. Tuna wakati sawa kila siku wa kufanya yale ambayo yanatuhusu. Hali wengi wetu tunafikiri kwamba hatuna wakati wa kutosha kufanya kila kitu.

Sara amesema ukweli. Wakristo wana wajibu zaidi wa kupanga jinsi ya kutumia wakati wao kila siku. Hebu tusome maneno ya Yesu katika Yohana 9:4. Watu wengi hawamjui Kristo. Wakristo wengi wangali “watoto wachanga katika maisha ya Kikristo” (1 Wakorintho 3:1). Wanahitaji mtu wa kuwasaidia kukua katika uhusiano wao na Mungu. Kuna watu wengi wenye shida ambao wanahitaji kusaidiwa na marafiki Wakristo. Mchungaji wa Sara aliombea shida na matatizo yanayowapata Wakristo kila siku. Je, tunawezaje kufanya uamuzi wa busara tunapotumia wakati wetu?

“Ninajua Mambo Niliyowapangia”

Jibu ni rahisi sana, hali wengi hawaliamini. Tutaweza kufanya mengi zaidi tunapochukua muda kila siku wa kuwa peke yetu na Mungu. Je, inawezekanaje hivyo? Pia, jibu lake ni rahisi. Hebu tusome pamoja Kifungu cha Kukumbuka cha leo, Mithali 3:6.

Mungu atatuonyesha njia tunapomkumbuka katika kila jambo tunalofanya. Anajua yaliyomema kwetu. Anasema katika Yeremia 29:11 kwamba, “Ninajua mambo niliyowapangia.” Pia, katika Isaya 48:17 anasema kwamba, “Mimi ndimi Mwenyezi-Mungu, Mungu wako; ninayekufundisha kwa faida yako, ninayekuongoza katika njia unayotakiwa kwenda.”

Je, Mungu hutufundisha na kutuongoza vipi? Hutumia Roho Mtakatifu kuzungumza nasi tunapoomba na tunaposoma Neno lake. Hebu tusome jibu la Yesu katika Yohana 14:16-17; 16:13-15. (Soma vifungu hivi.)

“Nimeikamilisha Ile Kazi”

Je, umewahi kuwaza hivi? *Sina muda zaidi. Ninafanya kazi masaa mengi kutafutia jamaa yangu chakula. Hunichukua muda mrefu kwenda na kurudi kutoka kazini. Wengine hawanikubalii nitumie wakati wangu jinsi ninavyotaka.*

Wakristo wengi hupatwa na shida hizi. Je, tunawezaje kupata wakati wa kuwa na Mungu kila siku? Je, tunawezaje kupata wakati wa kupewa uongozi wake ili tuwe mawakili wema wa wakati wetu? Hebu tuone mifano iliyowekwa na mtu mmoja ambaye alikuwa na kazi nyingi.

Yesu alikuwa na kazi nyingi ya kufanya kwa wakati mfupi. Alizungumza na Baba yake kabla ya kushikwa na kusulibiwa. Hebu tusome sehemu ya ombi lake katika Yohana 17:1-4; 20-21. Ikiwe wewe ni Mkristo umejumlishwa katika “wote watakaoamini kutokana na ujumbe wao.”

Ni lazima tutambue kwamba sasa tunao wajibu wa kuwasaidia wengine kumwamini Yesu. Yesu alitumia wakati wake mwingi kuwaambia watu juu ya upendo na wokovu wa Baba yake. Hii pia itachukua wakati wetu mwingi. Ni lazima tuwe kama Yesu na tutumie wakati wetu vizuri. Nasi tunaweza kumwambia Baba yetu kwamba, “Nimeikamilisha ile kazi uliyonipa niifanye.”

“Nimekuja Kwa Sababu Hiyo”

Je, Yesu alimwambia nini Nikodemo katika Yohana 3:16? (Sema au soma kifungu hiki.) Yesu alijua kwa nini alikuja dunaini na yale aliyotakiwa kufanya kumaliza kazi hiyo. Alipangia wakati wake kwa kuwa na ufahamu huu.

Ni lazima tupange kufanya mambo muhimu kwanza ikiwa tunataka kutumia vizuri wakati wetu. Je, ni nini cha muhimu kwetu? Je, ningefanya nini kwa saa hii ambayo imepita, siku hii na mwaka huu? Je, ninapaswa kufanya nini ndipo nitimize haya yote?

Soma vifungu vifuatavyo na ujibu maswali haya:

- ❖ *Marko 1:35-38* Je, Yesu aliomba wakati gani? Je, alifanya mambo yote mema ambayo wafuasi wake walimwambia? Je, kwa nini?
- ❖ *Luka 6:12-13* Je, kulingana na kifungu hiki, Yesu aliomba wakati gani? Je, Yesu alifanya uamuzi upi baada ya kuomba?

Je, unaweza kuamka asubuhi kila siku? Je, unapaswa kukataa mambo mema ya kufanya? Je, huwa unatafuta mwongozo wa Mungu kabla ya kuamua kutenda? Uamuzi mzuri utakusaidia kutumia wakati mfupi baadaye.

Hebu tusome wakati mwingine ambao Yesu aliomba katika Luka 9:28-32. Je, watu wengine walikuwa wakifanya nini wakati Yesu alipokuwa akiomba? Yesu alikuwa na watu wengine, lakini aliomba peke yake. Je, unaweza kutumia wakati wako na wengine unaposafiri kuomba kimoyomoyo pale ulipo?

Mwanamke mmoja alitafuta sana mahali pa kuombea kila asubuhi. Watoto wake wadogo walijua wakati ambao aliamka na kutoka kitandani kwenda kuomba. Alimwomba Mungu amsaidie kupata wakati mzuri wa kukutana naye na kuomba. Aligundua kwamba huwa macho dakika thelathini kabla ya wengine kila asubuhi. Lakini sasa anaweza kuomba akiwa kitandani bila kulala.

“Waliokuwa Mezani Pamoja na Yesu”

Je, umewahi kusikia mtu akisema, “Nina kazi nyingi sana hata sina nafasi ya shuguli zingine?” Yesu alitumia wakati wake mwingi kuomba, kuhubiri, kufundisha na kuponya. Alikuwa na wakati wa kutembelea marafiki. Biblia inatuambia baadhi ya wakati ambao alikula na rafiki zake. Hebu tusome Yohana 12:1-2.

Yesu alikuwa na wakati wa kupumzika. Marko 4:35-41 inatuambia kuhusu wakati Yesu alipotuliza dhoruba. Je, unakumbuka Yesu alikuwa akifanya nini wakati wanafunzi wake walipokuwa na hofu juu ya dhoruba? (Wape muda wa kujibu.) Mathayo, Marko, Luka na Yohana huwa wanaandika kwamba Yesu aliuacha umati wa watu na akaenda kuwa peke yake au pamoja na wafuasi wake wachache.

Kiongozi: Yesu aliwaahidi wafuasi wake ahadi maalum kuhusu uwezo wao wa kufanya kazi ya Mungu. Hebu tusome Yohana 14:12.

Shida nyingi tunazozipata kuhusu utumiaji wa wakati wetu zitajibiwa ikiwa tutaombea Wakristo wengine kama Paulo. Hakuomba juu ya utumiaji wa wakati wao, hali ombi lake lingetumiwa na wote ambao wanataka kumtumikia Mungu kila siku. (Soma Wakolosai 1:9-14.)

Tunapomalizia, hebu tuombe kwamba tutajazwa na hekima ya mapenzi ya Mungu na ufahamu ambao Roho wake hupatiana. Omba kwamba kila mmoja wetu ataweza kuishi jinsi Mungu anavyotaka na atafanya kila wakati yale yanayo mpendeza. Kisha maisha yetu yataonyesha kila hali ya matendo mema na tutakua katika ufahamu wetu wa Mungu.



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Mithali 16:1-9; Siku ya 2) Mhubiri 3:1-8; Siku ya 3) Mhubiri 3:9-22; Siku ya 4) Mhubiri 8:1-8; Siku ya 5) Kutoka 20:1-11; Marko 2:23-28; Siku ya 6) Yohana 17:1-12; Siku ya 7) Yohana 13-26

Somo la Sita

Itumieni Miili Yenu kwa Ajili ya Kumtukuza Mungu

Maandiko ya Biblia: 1 Wakorintho 6:12-20; Waefeso 4:17-5:20

Kifungu cha Kukumbuka: *"Namwomba Mungu, kadiri ya utajiri wa utukufu wake, awajalieni kwa uwezo wa Roho wake, nguvu ya kuwa imara ndani yenu."*
Waefeso 3:16

Mariamamu alipata Biblia yake chini ya sanduku lake la zamani la shule. Alikuwa ameiweka hapo tangu alipomaliza mtihamu wake wa somo la Biblia. Alishangaa jinsi alivyoweza kupata kwa urahisi vifungu vya Biblia wakati mhubiri wa redioni alipokuwa akisema. Miaka miine ilikuwa imepita tangu aache kugusa Biblia. Machozi yalianza kumtoka alipokuwa akisoma 1 Wakorintho 6:19-20. (Soma vifungu hivi.)

"Mwili wangu si *hekalu la Roho Mtakatifu*" Mariamamu akaema. "Mungu hawezi kusema hivyo kuhusu mwili wangu! Mwili wangu umetumiwa kwa mambo mengi katika miaka michache iliyopita, lakini hakuna lile ambalo lilikuwa la kumtukuza Mungu."

Somo hili ni kwa watu kama Mariamamu. Limeandikiwa pia Wakristo waliokomaa ambao wanapaswa kufikiria tena juu ya maana ya 1 Wakorintho 6:19-20. Miili yetu ni zawadi kutoka kwa Mungu. Ikiwa tunataka kuwa mawakili wema wa vipaji vyote vya Mungu, ni lazima tufikirie kifungu hiki.

"Kama Unavyojipenda Wewe Mwenyewe"

Kabla ya kujifunza kifungu kilicho hapo juu, tunapaswa kuanza na kifungu kingine ambacho kinafanana na hicho, ambacho huwa hakisomwi chote. Wakristo wengi wamejifunza kwa moyo jibu la Yesu kwa swali hili, "Je, ni amri ipi iliyo kuu?" Lakini wamesahau sehemu moja ya kifungu kinachofuata. Hebu tusome jibu lote la Yesu katika Mathayo 22:37-39.

Wakati mwingi Wakristo hawawapendi jirani zao, lakini wengi watakubali kwamba tunapaswa kuwapenda. Hii si sehemu ya kifungu cha 39 ambacho Wakristo wengi husahau. Je, Yesu alisema tunapaswa kuwapenda vipi jirani zetu? Ikiwa Wakristo wengi wangewapenda jirani zao jinsi wanavyojipenda, *ingekuwa* kidogo sana. Baadhi ya Wakristo wanajishughulisha na kuwajali wengine mpaka hawajitunzi vizuri wao wenyewe. Weninge wanaamini kwamba wao si watu wa thamani au muhimu.

Hebu kwanza tuachie hapo na tuombe. Jibu maswali yafuatayo na uchukue wakati mfupi kumwambia Mungu majibu yako:

❖ Je, unajipenda kweli?

❖ Je, unawajali na kuwatumiza wengine jinsi unavyojijali?

❖ Je, unafikiri wewe ni wa Muhimu kwa Mungu kama watu wengine?

(Mwambia mmoja aombe kwamba kila mmoja katika kundi hili atajifunza leo mengi zaidi kuhusu thamani yao kama wana wa Mungu.)

“Hekalu la Mungu” na “Vyombo vya Udongo”

Hebu tuangalie kwa makini mwanzo na mwisho wa 1 Wakorintho 6:19-20. Paulo aliandika kwamba, “Miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu.” Alimalizia maneno yake kwa waamini kwa kusema kwamba, “Itumieni miili yenu kwa ajili ya kumtukuza Mungu.”

Wasomaji wa Paulo walijua kusudi la hekalu siku zao. Kulingana na dini nyingi, kulikuwa na sheria kali jinsi hekalu lilipaswa kujengwa. Palikusudiwa kuwa nyumba ya muungu na kutumiwa kwa ajili yake. Ilijengwa kumheshimu na kumtukuza muungu wao. Hekalu hujengwa ili kutumiwa kumshimu yule aliyejengewa, sio wale wanaoabudia pale.

Katika 2 Wakorintho 4:7, Paulo anaelezea Wakristo kwa kutumia neno lingine ambalo halionekani kuwa la heshima. (Soma 2 Wakorintho 4:1-2, 7.) Unapaswa kujibu maswali haya moyoni mwako. Tumia dakika chake kuomba na kumwambia Mungu majibu yake.

❖ Je, watu wanapo niangalia, wananiona mimi au wanamwona Mungu ndani yangu?

❖ Je, ninamtumikia Mungu kwa utukufu wake au kwa utukufu wangu?

❖ Je, ninampatia Roho Mtakatifu wa Mungu mahali pazuri pa kuishi?

(Mwambia mmoja wao afunge kwa maombi baada ya kuuliza swali la mwisho. Waambie waombe kwamba, tuweze kukua katika uwezo wetu wa kumtumikai na kutumiwa na Mungu.)

“Itumieni Miili Yenu kwa Kumtukuza Mungu”

Hekalu za siku za Paulo zilipaswa kuwekwa safi na takatifu. Mungu alitumba na akampa kila mmoja wetu mwili. Ni lazima tuiweke miili yetu kuwa safi na takatifu tayari kutumiwa. Hii inamaana kwamba ni lazima tupumzike ya kutosha na tule chakula kizuri. Ni lazima tujitunze tunapokuwa wagonjwa. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunakunywa maji safi. Ni lazimu tujitunze jinsi tunavyowatumiza watu tunao wapenda.

Wakili Mkristo anapaswa kuweza kusema kwa uaminifu, “Mwili wangu ni zawadi kutoka kwa Mungu. Ninapaswa kuutumia kumtumikia. Ninapaswa kutumia mikono yangu kufanya kazi yake. Ninapaswa kutumia miguu yangu kwenda kule anakotaka niende. Ni lazima niutunze mwili wangu na niutayarishe kufanya kazi. Ikiwa

nitakuwa mdhaifu au mchafu kwa njia yo yote, itadhuru uwezo wangu wa kufanya kazi yake.”

Watu wa kwanza kupokea barua za Paulo walikuwa Wakristo wapya. Walikuwa na mengi ya kujifunza kuhusu uhusiani wao mpya ambao watakuwa nao na Mungu kupitia kwa Mwanawe, Yesu Kristo. Tuseme pamoja Warumi 12:1, Kifungu cha Kukumbuka cha Soma la Nne.

“Nyinyi Ni Watoto Wake Wapenzi”

Unapompokea Kristo kuwa Mwokozi wako, unafanyika kiumbe kipya, lakini ni lazima tuamue kutokuwa watumwa wa dhambi. Hebu tusome maelezo ya Paulo ya jambo hili katika Warumi 6:6; 12-14.

Tumeangalia kwa makini 1 Wakorintho 6:19-20. Paulo alikuwa amepeana *picha* ya kile kinachofanyika wakati Mkrsito anapofanya dhambi kabla ya kuandika maneno haya. (Soma 1 Wakorintho 6:15-17.)

Ikiwa Roho Mtakatifu wa Mungu yuko daima ndani yetu, basi yuko pale. tunapofanya dhambi. Dhambi yetu hutudhuru. Dhambi hudhuru uhusiano wetu na Baba. Paulo aliandika kwamba, “Kwa hiyo, mwigeni Mungu, maana ninyi ni watoto wake wapenzi” (Waefeso 5:1). Tunapofanya dhambi, huwa hatuwi kama Mungu. Ushuhuda wetu si kama wa mtoto ambaye anamheshimu na kumtukuza Baba yake.

Paulo aliwaandikia barua Waefeso karibu miaka 2000 iliyopita, lakini inaonekana kama kwamba iliandikwa jana. Ugonjwa kama UKIMWI umewaua Wakristo wengi miaka kadhaa iliyopita. Hebu tusome Waefeso 5:3-5.

“Kuwa Watu Safi, Wasio na Lawama”

Je, unawaza kwamba, “Mimi si mtumwa wa dhambi hizi?” Hebu tusome zaidi yale ambayo Paulo alifikiria kuwa dhambi ambayo inawazuia Wakristo kutokuwa wenye hatia na haki kama watoto kamilifu wa Mungu. Soma vifungu vifuatavyo na ukamilishe sentenzi hizi:

- ❖ *Wafilipi 2:14-16* “Fanyeni kila kitu bila _____.”
- ❖ *Wakolosai 3:8* “Lakini sasa mnapaswa kuachana na mambo haya yote: _____.”
- ❖ *Wakolosai 3:9* “Msiambiane _____.”
- ❖ *Waefeso 4:29* “Maneno _____ hata yasisikike kamwe miongoni mwenu.”

Yesu akawaambia, “Maana mtu husema kutokana na yale yaliyojaa moyoni” na “kwa maneno yako utahukumiwa kuwa na hatia” (Mathayo 12:34 37). Maneno yako yote yanaonyesha kwamba moyo wako umejaa upendo na uongozi wa Mungu?

“Kuwa na Utaratibu na Kukesha”

Mawazo yetu yanapaswa kuwa kama ya mtoto wa Mungu jinsi ilivyo na maneno yetu. Katika Mathayo 15:19, Yesu alisema, “Maana moyoni hutoka mawazo” mabaya. (Soma Waefeso 4:23-24.)

Petro wa Kwanza 4:7 inasema, “Kwa hiyo mnapaswa kuwa na utaratibu na kukesha ili mweze kusali.” Maombi ni njia ya kuzungumza na Baba. Ni njia ambayo tunajua mapenzi yake na kumwomba atuongoze.

Wakati mwingi huwa hatuna akili safi kwa sababu ya kuiga marafiki zetu. Tunaweza kuwa marafiki wa wale ambao hawamjui Kristo kama Mwokozi ikiwa tunataka kuwashuhudia. Lakini hatupaswi kufuata njia zao wala kuwa kama wao. (Soma Wafilipi 3:17-21.)

Tunao wajibu pia wa kuwafundisha watoto na vijana wetu kufanywa wapy katika roho na nia zao. Ni lazima tuwafundishe kwamba miili yao ni zawadi kutoka kwa Mungu. Ni lazima tuwahakikishie kwamba njia za desturi zetu ni njia za Mungu. Tunaweza kuwa tukiwahimiza kupitia kwa desturi zetu kufanya yale ambayo hayamtukuzi Mungu. Tunaweza kuwa tukiwahimiza kuishi kama watu waovu na wenye dhambi badala ya kuwa watoto watakatifu wa Mungu (Wafilipi 2:15).

Ni lazima mawakili Wakristo wawafundishe watoto na vijana katika nyumba zao na makanisani juu ya mambo kama ngono na UKIMVI. Ni lazima tuwafundishe yale ambayo Mungu anafundisha juu ya jambo hili na sio ulimwengu.

Kiongozi: Tunaweza kuwa mawakili wema wa mwili wetu ikiwa tutamruhusu Mungu atusaidie kuwa *wenye nguvu ndani yetu*. Tunaweza kushinda dhambi na mamlaka yake juu yetu kwa kutumia nguvu za Mungu. Paulo alisema katika Wafilipi 4:7 kwamba amani ya Mungu italinda mioyo na akili zetu katika Kristo.

Ni lazima tumruhusu *Kristo awe na makao mioyoni mwetu* na atawale kila tendo na mawazo yetu. Ni lazima tutafute msaada wake ili tuweze kung'ara kama nyota na *kupeana ujumbe wake wa uzima*. Hebu tusome Waefeso 3:16-17 ma Wafilipi 2:14-6, kabla ya kufunga kwa maombi.



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Waefo 3:14-21; Siku ya 2) Waefeso 4:17-32; Siku ya 3) Waefeso 5:1-17; Siku ya 4) Waefeso 5:19-33; Siku ya 5) Wafilipi 3:12-21; Siku ya 6) 2 Wakorintho 3:1-6, 12-18; Siku ya 7) Mathayo 12:33-36

Mali Yangu na Moyo Wangu

Maandiko ya Biblia: Mathayo 6:19-34; 19:16-24

Kifungu cha Kukumbuka: “*Maana pale ilipo hazina yako, ndipo pia utakapokuwa moyo wako.*” Mathayo 6:21

Ann alipokuwa mtoto, alichanganyikiwa na Zaburi 37. Zaburi hii inaahidi kwamba watenda mabaya wataadhibiwa pamoja na maskini “wataimiliki nchi, hao watafurahia wingi wa fanaka” (kifungua 11). Ann alikuwa amefundishwa kwamba Biblia yote inasema ukweli, lakini Zaburi 37 ingekuwaje inasema ukweli?

Majirani wengi wa Ann walikuwa wafanya kazi wa mashamba. Alijua kwamba wengi wao walitendewa vibaya na wenye mashamba. Wenye mashamba hawa walikuwa na nyumba kubwa na nguo nzuri. Majirani wa Ann walikuwa maskini na walihitaji vitu vingi. Je, kwa nini hawakutimiziwa hitaji la moyo wao la kuwa na nyumba nzuri, mavazi na chakula? Walikuwa wao na siyo wenye mashamba ambao walimtumaini Bwana na wakatenda mema (vifungu vya 3-4).

Miaka mingi baadaye Ann alijifunza kwamba hazina iliyoahidiwa katika Zaburi 37 haikuwa hazina ya hapa duniani. Hazina tofauti imeahidiwa kwa wale ambao watamtumikia na kumtii Mungu. Amani iliyoahidiwa inaweza tu kutoka kwa hazina kama hii, wala si hazina ya hapa duniani. Zaburi hii inafundisha kuhusu hali ya moyo na akili ambayo Mungu anatarajia kutoka kwa watoto wake. Hii ndiyo hali ambayo tunaweza kuwa nayo ikiwa tutavaa “hali mpya ya utu ambayo imeumbwa kwa mfano wa Mungu.” (Soma Waefeso 4:22-24.)

Tutajifunza leo jinsi ya *kuacha tamaa mbaya za utu wetu wa kale* ambazo hudhuru uwakili wa vitu tulivyonyavyo. Tutajifunza yale ambayo Yesu alifundisha wafuasi wake wakati tunapojibu maswali haya: Je, ninapaswa kuwa na hali gani ya moyo na mawazo juu ya hazina ya duniani? Je, ni hazina zipi ambazo moyo wangu unatamani?

“Utakuwa na Hazina Mbinguni”

Yesu akawaambia, “Ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita katika tundu ya sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni” (Mathayo 19:24). Je, Yesu aliamini kwamba ni vibaya kuwa tajiri? La! alielewa kwamba watu wachache wana nia njema juu ya hazina ya duniani. Alijua pia kwamba nia mbaya humfanya mtu atende dhambi.

Hebu tusome hadithi yote kuhusu yule tajiri. (Soma Mathayo 19:16-24.) Je, mtu huyu alisema amri zote kumi? La! Hakusema ile inayosema, “Usitamani nyumba ya jirani yako . . . wala chochote kilicho mali ya jirani yako” (Kutoka 20:17). Yesu alijua kwamba shida ya mtu huyu haikuwa pesa zake au mali. Shida yake ilikuwa nia mbaya kuhusu mali yake.

Mtu huyu alitaka kuwa tajiri na kuwa na mali yote ambayo matajiri huwa nayo. Hakukubali pesa na mali yake kuwa zawadi kutoka kwa Mungu. Hakujiona kuwa na wajibu wa kutumia mali yake kumtumikia Mungu.

“Hazina . . . Moyo Wako”

Mtu huyu tajiri alipaswa kuchagua kati ya hazina ya dunaini na hazina ya mbinguni. Yesu anawauliza swali hili wafuasi wake wa siku hizi. Hatuambii tuache vitu vyote ambayo tunaweza kutumia pesa kununua. Anasema kwamba ni lazima tuchague kilicho cha muhimu kwetu. (Soma Mathayo 6:19-21.)

Usijibu kwa sauti maswali haya. Ni lazima uyajibu moyoni mwako na uzungumzane na Mungu. Hebu tufumbe macho yetu. Omba kimoyo moyo baada ya kusomwa kwa kila swali. (Mwombe mungu awaongoze mnapoendelea na somo hili, baada ya kuuliza swali la mwisho.)

- ❖ Je, ninajiwekea hazina hapa duniani ili nitumie au kuwaonyesha watu mali niliyo nayo?
- ❖ Je, ni hazina ipi iliyo ya muhimu kwangu?
- ❖ Je, ninakubali kuwa vyote nilivyo nayo ni zawadi kutoka kwa Mungu? Je, ninatumia vyote anavyonipatia kumtumikia? Je, mimi ni wakili mwema wa zawadi zake?

“Kutumikia Mabwana Wawili”

Watumwa humfanyia kazi bwana wao. Nyumba, pesa na mavazi si watu, hali tunaruhusu vitu hivi kuwa mabwana wetu. Tamaa ya kupata vitu fulani inaweza kutawala maisha yetu. Hivi ndivyo Yesu alifundisha katika Mathayo 6:24. (Soma kifungu hiki.)

Yesu, kabla ya kuwatuma wanafunzi wake kwenda kuhubiri na kufundisha, alisema, “Ampendaye baba au mama yake kuliko anipendavyo mimi, hanistahili.” (Soma Mathayo 10:37.) Je, kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi wake hivyo? Alijua kwamba huwa tunaruhusu jamaa zetu, nyumba, kazi na hata kanisa kuwa mabwana zetu.

Yesu alijua kwamba baadhi ya wanafunzi wanataka kuacha jamaa zao. Jamaa zao wanaweza kuwatatanisha wanapoondoka kwa muda

mrefu. Wengine wanaweza kuhofia kushikwa na magonjwa ya wale wanaowatumikia. Yesu alikuwa akisema kwamba, *Mungu ndiye bwana wenu. Msitumie jamaa zenu, marafiki, kazi au kanisa kama sababu ya kutofanya mapenzi ya Mungu. Jiulize maswali haya:*

- ❖ Je, kati ya mali niliyo nayo hapa duniani, ni ipi iliyo ya muhimu kwangu? Je, ninaweza kuwa tayari kuuza vitu hivyo na nimpatie Mungu pesa hizo? Je ninaweza kufanya hivyo kwa furaha?
- ❖ Je, niko tayari kuiacha jamaa yangu au kazi yangu kwenda kuongoza masomo ya Biblia au kushuhudia?
- ❖ Ikiwa Mungu ataniuliza, utasaidia watu wenye ugonjwa wa UKIMWI? Je, ninahofu ya kuambukizwa au kuwaambukiza jamaa yangu ugonjwa huu?
- ❖ Je, ninaweza kuwahimiza watoto wangu kufuata mapenzi ya Mungu hata ikiwa watalazimika kuondoka nyumbani au kwenda kuishi sehemu nyingine?
- ❖ Je, ninaweza kuacha kanisa langu na kuanzisha kanisa katika sehemu nyingine?

“Msiwe na Wasiwasi”

Bila shaka wafuasi wa Yesu walishangaa sana wakati alipowaambia, “Msiwe na wasiwasi juu ya chakula na kinywaji mnavyohitaji ili kuishi, wala juu ya mavazi mnayohitaji kwa ajili ya miili yenu.” Pengine walifikiri kwamba, “Anajua tunahitaji vitu hivi, je, kwa nini anatuambia tusivisumbukie?” Tunaweza kupata jibu katika yale ambayo Yesu alisema baadaye. (Soma Mathayo 6:25-34.)

Yesu alijua kwamba kuna tofauti kujua hitaji na kufadhaika. Si kosa kuchukua wajibu wa kutimiza mahitaji yetu, lakini kusumbuka hakutimizi mahitaji yetu. Kusumbuka husababisha huzuni na mtu mwenye huzuni hawezi kufanya uamuzi mwema wala kutenda mema.

Je, mtu anawezaje kutosumbuka? Yesu anatumkumbusha kwamba tunapaswa kujishughulisha na vitu vinavyostahili. Hatutakuwa na wakati wa kusumbuka ikiwa tunajishughulisha na kumtumikia Mungu. Hatutakuwa na wakati wa kusumbuka ikiwa tunamwamini Mungu wetu mkuu na mwenye hekima.

“Dini Humfanya Mtu Tajiri Sana”

Yesu anasema katika Mathayo 6:32-33 kwamba Mungu anajua tunahitaji chakula, maji na nguo “na hayo yote mtapewa kwa zaida.” Kuna watu wengi katika nchi yetu ambao hawatamani kuwa na chakula kingi, maji na mavazi. Lakini wanataka tu chakula cha kutosha, maji na mavazi ya kuwasaidia kuendelea kuishi. Watu hawa wengi wanampenda na wanamwamini Mungu.

Hapa tunapata swali kuu sana ambalo waalimu wa kidini hubishana sana. Je, kwa nini Mungu anawaruhusu baadhi ya Wakristo kuteseka hali waovu wanakuwa matajiri? Waalimu wa Agano la Kale wa wakati wa kanisa la kwanza walibishana pia kuhusu swali hili. Baadhi yao walifundisha kwamba Wakristo wote watakuwa matajiri. Paulo aliandika katika 1 Timotheo 6:6 kwamba, “Kweli dini humfanya mtu awe tajiri sana, ikiwa anatosheka na vitu alivyo navyo.”

Yesu alisema katika Mathayo 6:25 kwamba, “Je, maisha ni chakula tu au zaidi? Na mwili, je, si zaidi ya mavazi?” Watu wanaoishi duniani wanahitaji chakula na mavazi, lakini hizi si utajiri mkubwa. Utajiri mkubwa ni ahadi ya uzima wa milele na amani ambayo Wakristo peke yake hupata.

Je, ni kosa kwa mawakili Wakristo kuuliza, “Je, hazina yangu ni gani hapa duniani?” La! ikiwa watauliza pia, “Je, ninawezaje kutumia hazina hii kumtumikia Mungu?” Hebu tusome tena Mathayo 6:33 na tujibu maswali haya: (Wape muda kila mmoja kusema kimoyo moyo na Mungu baada ya kuuliza kila swali.)

- ❖ Je, kuna watu ambao hawana chakula, maji na mavazi kwa sababu sijawahi kuwa wakili mwema wa mali yangu?
- ❖ Je, nina hazina ambayo nimejiwekea duniani ambayo ninapaswa kutumia na wengine?

Kiongozi: Hebu tufunge somo la leo kwa kusoma vifungu vifuatavyo na kujibu maswali yafuatayo:

- ❖ *1 Timothy 6:9-10* Je, hazina na utajiri vimenifanya nipoteze imani yangu kwa Mungu?
- ❖ *Wafilipi 4:12-13* Je, nimetosheka na utajiri wangu hapa duniani iwapo ni kidogo au nyingi? Je, ninategemea nguvu ambayo Mungu ananipatia?
- ❖ *Yakobo 2:14-17* Je, vitendo vyangu vinathibitisha imani yangu?
- ❖ *1 Yohana 3:17-18* Je, mali na hazina yangu imeufanya moyo wangu kuwa mgumu?

Uwe na wakati juma hili kufikiria tena maswali haya ambayo umeulizwa leo. Hebu kila mmoja wetu aombe sasa na kila wakati kwamba tutakuwa mawakili wema wa vyote ambavyo tumepewa na Mungu.



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Zaburi 37:1-13; Siku ya 2) Zaburi 37:14-29; Siku ya 3) Zaburi 37:30-40; Siku ya 4) 1 Timotheo 6:1-10; Siku ya 5) Wafilipi 4:1-20; Siku ya 6) Yakobo 2:14-26; Siku ya 7) 1 Yohana 3:16-24

Zaka na Dhabihu Zenu

Maandiko ya Biblia: Malaki 3:6-18; 2 Wakorintho 8:1-9:15

Kifungu cha Kukumbuka: *"Kila mmoja, basi, na atoe kadiri alivyoamua, kwa moyo na wala si kwa huzuni au kwa kulazimishwa, maana Mungu humpenda yule mwenye kutoa kwa furaha."* 2 Wakorintho 9:7 (Ikiwa unataka kujifunza kwa ukamilifu sehemu hii ya uwakili, anza na somo lililotayarishwa mnapokutana mara ya kwanza. Malizia somo hili katika mkutano wa pili. Kisha someni, jadilianeni na muombe kwa kutumia 2 Wakorintho 8 na 9.)

"Susana, kuna tatizo lo lote?" Anna alimwuliza rafiki yake. "Ulionekana mwenye mawazo mengi wakati wa kujifunza somo la uwakili kutoka kwa *Iwe Nuru*."

"Utadhanja kwamba mimi ni mpumbavu," Susana akamwambia. "Ninalokumbuka kwa mara ya kwanza ni kwamba baba yangu akinipa pesa kidogo Jumamosi moja na kuniambia, 'Wewe umefika umri wa kubadilisha pesa za kutoa zaka.' Mtoto ndiye alieenda dukani kila Jumamosi kubadilisha shilingi na kuleta senti za kutoa. Kisha, kila Jumamosi baba yangu aliweza kutugawia senti hizi mimi na dada zangu ili tukatoe kanisani."

"Mimi nimekuwa nikitoa kanisani na pia ni mwalimu wa hesabu, lakini bado sijaelewa utoaji wa zaka. Je, ninatoa sehemu ya kumi ya pesa ninazopata kabla au baada ya kutolewa ushuru?"

Je, utamjibu vipi Susana? Tunaweza kuwashauri na kuwaongoza wengine. Lakini hatuwezi kuwajibu maswali yao kuhusu kumtolea Mungu sadaka. Mungu aliwaamuru watoto wake wote kutoa zaka, lakini si jambo ambalo linaweza kuamuliwa kwa kutumia hesabu. Kutoa zaka ni amri ambayo ni lazima tutii kwa sababu mioyo yetu imejaa nia ya kutakakutumika, kumheshimu na kumshukuru Mungu. Hebu tusome Kumbukumbu la Torati 14:22-23.

Kukamilisha Mafundisho Yao

Watu wa Agano la Kale walitii amri za Mungu kwa kuhofu ya kuadhibiwa. Walizitii kama sheria kali sana. Sisi tunamwamini Yesu Kristo. Tuna uhusiano mpya na Mungu.

Je, unakumbuka maneno ya Yesu katika Mathayo 5:17? (Sema au soma vifungu hivi.) Yesu alikuja kutusaidia kuelewa jinsi ya kutii amri na sheria zote kama watu ambao wamekubali upendo na wokovu wa Baba yake. Hebu tusome vifungu vifuatavyo na tujibu maswali haya:

- ❖ *Mathayo 23:23* Je, watu hawa walitii amri ya kuto zaka? Je, walitii amri zote za Mungu? Je, unafikiri walitii kwa sababu walimpenda na kutaka kumtumikia Mungu?
- ❖ *Luka 18:9-14* Je, ni yupi kati ya watu hawa wawili alikuwa na uhusiano mwema na Mungu? Je, unafikiri Mfarisayo alitoa zaka yake kwa sababu alimpenda na alitaka kumtumikia Mungu?

“Huku Mnaacha Mambo Muhimu ya Sheria”

Je, Yesu alijibu nini alipoulizwa, “Ni amri ipi iliyo kuu katika sheria?” (Mwambie mmoja wao aseme au asome Mathayo 22:37-40.) Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kwamba, “Sheria yote ya Mose na mafundisho ya manabii vinategemea amri hizi mbili.” Haya ndiyo aliyokuwa akirudia katika Mathayo 23:23. (Soma tena kifungu hili.)

Sio kosa kutoa zaka na sadaka kwa kanisa letu. Lakini Mungu anataka tufanye mambo haya yote kwa sababu tunampenda kwa mioyo yetu yote, roho na akili. Anataka sadaka zetu kwa sababu tunataka kumheshimu na kumshukuru kwa zawadi zake zote kwetu.

Je, waalimu na Mafarisayo walikuwa wakipuuzwa sheria zipi? (Wape muda wa kujibu.) Mtu ambaye kweli anampenda Mungu atatii sheria zinazohusu haki, rehema na uaminifu. Mtu ambaye anampenda jirani yake atatii sheria hizi.

“Msitende Dhambi”

Je, kwa nini tunawapa watoto sheria? Je, kwa nini seriakli yetu ina sheria? Je, tungehitaji sheria hizi ikiwa watu hawafanyi mambo ya kuwadhuru wao wenyewe na wengine? Sheria zinazofaa hutolewa kutusaidia, kutuongoza na kutulinda wakati tunaposhindwa au tunapokosa kujifanyia mambo haya.

Tunahitaji sheria kwa sababu huwa tunaamua kufanya yale yanayotudhuru sisi wenyewe na wengine. Tunahitaji sheria kutuongoza katika kutenda kazi fulani. Mungu alijua hivyo alipowapa watu wa Agano la Kale sheria na mafundisho yake. Hebu tusome yale ambayo Musa aliwaambia watu baada ya kupewa Amri Kumi. (Soma Kutoka 20:18-21.)

Sheria na amri nyingi huandamana na adhabu. Adhabu hii ipo ili kutuhimiza kutii sheria ambazo zinatufaa sisi na watu wengine. Adhabu hii huwa ndogo kulingana na madhara na uchungu tunaajiletea sisi wenyewe na watu wengine tunapotii sheria na amri.

“Nitakupa Sehemu ya Kumi”

Je, kuna sheria na mafundisho yapi katika Agano la Kale yanayohusu zaka na sadaka? Soma vifungu hivi na ujibu maswali yafuatayo:

- ❖ *Mwanzo 14:18-20* “Abramu akampa Melkizedeki (kuhani wa Mungu Mkuu) mchango wake sehemu ya _____ ya vitu vyote alivyokuwa navyo.”
- ❖ *Mwanzo 28:22* “Nami nitakupa sehemu ya kumi ya vitu vyote _____.”
- ❖ *Hesabu 18:25-26* “Mtanitolea mimi Mwenyezi-Mungu sehemu moja ya _____ ya zaka hiyo.”
- ❖ *Mambo ya Walawi 27:30-32* “Zaka na mazao iwe ni nafaka au matunda ya miti; yote ni mali ya _____.”
- ❖ *Malaki 3:8-12* “Leteni ghalani mwangu _____ yote, ili nyumbani mwangu kuwe na chakula cha kutosha.”

Tumezungumzia kuhusu adhabu ambayo mtu hupata anapokosa kutii sheria. Kunazo baraka wakati mtu anapotii sheria! Mungu hutupatia sheria, amri na mafundisho kutubariki na kutusaidia. Soma tena Malaki 3:10-12.

“Habari Juu ya Neema Ambazo Mungu Ameyajalia”

Yesu alifundisha mengi kuhusu uhusiano mpya ambao tunaweza kuwa nao na Baba. Je, tunayafanyaje mafundisho yake yawe sehemu ya maisha yetu? Wakristo wa Kwanza walipata uongozi na himizo kutoka kwa Paulo, mtumishi wa Mungu aliye chaguliwa. Tunaweza kufanya hivyo pia. Hebu tusome baadhi ya majibu na mifano inayopatikana katika barua zake:

- ♦ Wakristo waliaamini kwamba kwa kuwa Mungu alikuwa amewapatia zaidi, walikuwa na wajibu wa kutimiza mahitaji ya wale ambao hawana. Hawakujaribu kugawa kiasi sawa kati yao. Walihakikisha kwamba kila hitaji lilitimiziwa. Walishiriki zaidi ya mali yao tu. Tunaweza kutoa arthi kwa ajili ya kanisa letu. Tunaweza kuwagawia wengine mboga tunazokuza katika mashamba yetu. (Soma Matendo 2:43-47.)
- ♦ Baadhi ya watu, kama wakulima wa kahawa, hulipwa mara moja au mara mbili kwa mwaka. Watu wengi hupewa zawadi ya pesa kazini wafikapo mwisho wa mwaka. Paulo anatumia kumtolea Mungu sadaka kila Jumapili kulingana ya mapato yetu ya *juma hilo*. (Soma 1 Wakorintho 16:1-2.)
- ♦ Badala ya Paulo kutupatia orodha ya sheria za kuto, anatumia kuhusu “habari juu ya neema ambazo Mungu ameyajalia makanisa.” Anawakumbusha wasomaji wake kuhusu wokovu

unaopatikana kupitia kwa “neema ya Bwana wetu Yesu Kristo.” Paulo anaonyesha kile kinachoweza kufanyika ikiwa tutajitoa kwa Bwana. (Soma 2 Wakorintho 8:1-9.)

- ♦ Je, umetimiza ahadi zako zote kuhusu pesa na mali yako kwa kanisa lako na Mungu? (Soma 2 Wakorintho 8:10-12.)

“Kisha Mwaweza Kunijaribu”

Uwakili ni tendo la kuamini. Tutakuwa tayari kushiriki au kutumia anachotupatia Mungu ikiwa tunaamini kwamba yeye atatutunza. Ikiwa kweli tunampenda, tutataka kumrudishia zaidi ya fungu la kumi ambalo tumepokea. Hebu tusome ahadi maalum ya Mungu kwetu katika Malaki 3:10.

Paulo anataja njia nyingi ambazo Mungu hubariki utoaji wetu katika 2 Wakorintho 9. (Soma sentenzi hii, kisha usome vifungu hivi kutoka kwa sura hiyo.)

- ♦ Tunapotoa tunawahimiza wengine kutoa. (1 Wakorintho 9:1-2)
- ♦ Tunabarikiwa kulingana na jinsi tunavyotoa. (9:6-7)
- ♦ Tunabarikiwa tunapokuwa sehemu ya kufanya wengine wabarikiwe. (9:8-11)
- ♦ Watu wengine watamshukuru Mungu na kumtukiza wakati tunapowapatia vitu. Pia, tutapokea baraka za maombi yao. (9:12-15)

Kiongozi: Hatupaswi kutii amri ya Mungu ya kutoa kwa kutumia hesabu, bali kwa kutumia mioyo yetu. Sio amri ya kutuwekea mipaka, bali ni ya kutufanya tutumie vizuri mali yote aliyotupatia. Ni ukumbusho wa baraka na vitu vizuri anavyotaka kutupatia kwa wingi (Malaki 3:10).

Hebu tusome pamoja Kifungu cha Kukumbuka na kifungu kinachofuata cha 2 Wakorintho 9:7-8. Vifungu hivi vinapaswa kuwa mwongozo wa maombi yetu tunapomalizia somo la leo. Tunapotoa zaka na sadaka huwa tunamwonyesha Mungu jinsi tunavyomwamini na kumtegemea. Pia, ni njia ya kushuhudia wapotevu wanaotuzunguka juu ya upendo na wokovu wake.



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Kutoka 20:1-17; Siku ya 2) Kutoka 20:18-26; Siku ya 3) Mwanzo 28:10-22; Siku ya 4) Hesabu 18:25-32; Siku ya 5) Mambo ya Walawi 27:30-34; Siku ya 6) Kumbukumbu la Torati 14:22-29; Siku ya 7) Malaki 3:6-18;

Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma la Pili: Siku ya 1) Mathayo 23:23-28; Siku ya 2) Marko 12:13-17; Siku ya 3) Marko 12:38-44; Siku ya 4) Mathayo 6:1-4; Siku ya 5) Mathayo 16:1-12; Siku ya 6) Luka 16:1-15; Siku ya 7) Luka 16:19-31

Watoto Ni Zawadi Kutoka Kwa Mungu

Maandiko ya Biblia: Zaburi 127; Waefeso 6:1-4

Kifungu cha Kukumbuka: *“Watoto ni riziki kutoka kwa Mwenyezi-Mungu; watoto ni tuzo lake kwetu sisi.”* Zaburi 127:3

Jumapili moja, pale Parklands Baptist Church, Nairobi, mwanamke mmoja alishuhudia jinsi imani yake ya Kikristo imeathiri kazi yake maalum. Alipokuwa akizungumza, ilionekana wazi kwamba anapenda kazi yake sana. Amejitoa kufanya kazi yake kama mtumishi mwaminifu wa Mungu.

Phylis Maina amehitimu kama mwalimu kutoka chuo kikuu, lakini kazi yake muhimu sana ni ile ya kuwa mama. Somo hili, haliwahusu tu wazazi, linahusu yale aliyosema. Maneno yake yanaweza kusaidia Wakristo wote kutambua wajibu wao wa kuwa mawakili wema wa zawadi ya Mungu ya watoto.

“Mwenyezi-Mungu Asipoijenga Nyumba”

Zaburi 127:1 inasema, “Mwenyezi Mungu asipoijenga nyumba, waijengao wanajisumbua bure.” Sisi wote ni watu wenye shughuli nyingi, wenye kutofanya kazi bure. Huchukua juhudi kubwa kuwa na uhusiano na mtu mwingi. Hii ni pamoja na rafiki zetu, washiriki wa kanisa, majirani na jamaa zetu. Ni lazima tutafute msaada wa Mungu tunapofanya kazi ya kukuza uhusiano wetu. Hakuna lile ambalo litafanikiwa, Bwana asipokuwa katikati yake. Ni lazima tukubali kwamba hatuwezi kufanya lo lote wala kufanikiwa bila Mungu.

Bwana ametuambia wazi kwamba, tusipomshirikisha katika yale tunayofanya, iwapo ni uhusiano wetu, kazi, kitu cho chote maishani hatutavuna cho chote. Kamusi inasema kwamba maana ya neno bure ni kutokuwa na cho chote, bila kitu, pasipo cho chote. (Yohana 15:5.)

Mungu hutupatia ukweli na ni juu yetu kutii au kutotii. Anaahidi kutubariki tunapotii. Baraka mojawapo ambayo Mungu anatupatia ni watoto. Hatustahili wala si lazima tupate zawadi hii. Baraka hii ya watoto ni zawadi kutoka kwa Mungu.

“Watoto ni riziki kutoka kwa Mwenyezi-Mungu . . . Watoto walio na nguvu, ni kama mishale mikononi mwa askari. Heri mtu aliye na mishale hiyo kwa wingi” (Zaburi 127:3-5). Mungu ametupatia uhai wa watoto. Sisi ni mawakili wake. Tunaweza kupotosha mishale yetu

na tusifanye cho chote nayo, au tunaweza kuamua kumtii Mungu na tuwasaidie kwenda mahali ambapo Mungu angewataka waende.

“Lakini Kama Mmoja Wenu Ametindikiwa Hekima”

Mume wangu na mimi hatukujua kwamba tunaielewa machache sana kuhusu kuwa wazazi hadi wakati Mungu alipotupa watoto. Tulikumbuka jinsi tulivyokuwa tukiwapinga wazazi wetu na mambo waliyokosea. Kisha siku moja, tunaangalia furushi ndogo la furaha ambaye hajui cho chote kwamba hatujui cho chote kuhusu kuwa wazazi.

Kulingana na maisha ya kisasa, wamama wetu si majirani zetu. Tunakimbilia kwa maduka ya kuuza vitabu kusoma juu ya kutunza watoto. Mambo huwa mazuri mpaka mtoto anapoanza kuacha kutabasamu. Mtoto huyo huanza kutema mate, kutapika na kujifunza kukataa!

Jambo la kawaida ni kujaribu kwa mzazi kukasirika badala ya kutaka kuheshimiwa! Hii huendelea vizuri mpaka mtoto anapoanza kuuliza, *kwa nini?* Jibu la mzazi huwa kwamba, “Kwa sababu nimesema hivyo.”

Kisha nao watauliza, “Je, na wewe, ni nani hukwambia ‘nimesema hivyo?’ Ni nani anayekufanya *ukasirike* wakati unapokosa?” Maswali haya yote huwafanya watoto watake kujua ni nani anayekupa mamlaka ya kuwatawala.

Njia rahisi ni kuwaweka chini ya usimamizi mkali kwa kuwapa arodha ya mambo ya kufanya na yale ya kutofanya. Orodha hii itakuwa ya muda tu, lakini haitaathiri maisha yao au mtu watakaye kua na kuwa. Mungu anasema kwamba hatutafanikiwa ikiwa tutafanya hivyo kwa nguvu zetu. Ni lazima tumwalike atusaidie kwa kazi hii kuu. Anaweza kutupatia hekima tunayohitaji. (Soma Yakobo 1:5.)

“Nidhamu na Mafundisho ya Kikristo”

Biblia inasema, “Msiwachukize watoto wenu ila waleeni katika nidhamu na mafundisho ya Kikristo” (Waefeso 6:4).

Wakolosai 3:21 inasema, “Nanyi wazazi, msiwachukize watoto wenu, la sivyoyata tamaa.” Vifungu hivi vinaniambia, “Usiwasumbue watoto. Msumbue Mungu kwa ajili ya watoto hao! Mwombe kwa ujasiri kwa ajili yao.”

Mungu anatupa amri za kuishi kwa manufaa yetu katika Kumbukumbu la Tora 6:1-9. Hizi ni amri ambazo zina ahadi ya kuishi maisha marefu. (Soma kifungu hiki.)

Kuwaambia ukweli wa Mungu ni kazi ya siku zote. Ni lazima tufanye hivyo pale nyumbani, tunapotembea, tunapolala, tunapoamka asubuhi. Ni ishara inayoonekana kwa watu wote wewe kama mama. Vifungu hivi vinazungumzia hali yote ya maisha kwa sababu havizungumzii juu ya dini au mtindo fulani wa imani na kuabudu, lakini ni uhusiano.

Mungu anaahidi kwamba ikiwa tutawalea watoto kwa njia inayofaa, hawataiacha kamwe. Anatutarajia tuwafundishe watoto wetu vizuri wakiwa wangali wadogo wakati kuna tumaini. Tutaharibu maisha yao ikiwa hatutafanya hivyo. Mungu hutuadhibu kwa sababu anatupenda. Ni lazima pia tuwaadhibu watoto wetu ikiwa tunawapenda. Ni lazima tuwaongoze na kuwaelekeza kutii na kuwa na kiasi. Hebu tusome Mithali 19:18, 22:6 na Waebrania 12:5-6.

“Yesu Akaendelea Kukua Katika Hekima na Kimo”

Luka 2:52 inasema, “Naye Yesu akaendelea kukua katika hekima na kimo; akazidi kupendwa na Mungu na watu.” Wajibu wetu kama wazazi ni kuhakikisha kwamba watoto wetu wanafundishwa na kukua katika hali hizi nne:

- ♦ Kimwili – Ni lazima tuwasaidie wapate chakula bora, watunzwe na kupumzika ili miili yao iweze kukua.
- ♦ Kimawazo (Hekima) – Ni lazima tuwapatie nafasi ya kuweza kujifunza na kukua katika maarifa.
- ♦ Kijamii – Ni lazima tuwasaidie kukua katika kupendwa na watu
- ♦ Kiroho – Ni lazima tuwasaidie kukua katika kupendwa na Mungu

Pia, tuna wajibu wa kuwasaidia kujifunza kumtii Mungu, wazazi, wazee, na serikali. Hebu tusome 1 Petro 2:17.

Tunapotafuta kuwafundisha watoto wetu kumcha Mungu, ni lazima tutambue kwamba shetani ana mipango yake. Waefeso 6 inaeleza kwamba vita hivi ni vya kiroho. Sura hii inaanza kwa kuwaambia watoto kuwatii wazazi wao. Paulo aliandika kwamba, “‘Waheshimu Baba na mama yako,’ hii ndiyo amri ya kwanza ambayo imeongezewa ahadi.” Hebu tusome ahadi hiyo katika Waefeso 6:3.

Hatupaswi kufanya kazi ya kufundisha watoto, ili wawe na uhusiano mwema kwa kutumia nguvu zetu wenyewe. Paulo ameandika kwamba, “Hatimaye, nawatakeni mwe imara katika kuungana na Bwana na kwa msaada wa nguvu yake kuu. Vaeni silaha anazowapeni Mungu mpate kuzipinga mbinu mbaya za Ibilisi” (Waefeso 6:10-11).

“Salini Kila Wakati”

Baada ya Paulo kuorodhesha silaha ya Mungu, aliandika kwamba, “Salini daima, mkiomba msaada wa Mungu. Salini kila wakati kwa nguvu ya Roho. Kesheni bila kuchoka mkisali kwa ajili ya watu wote wa Mungu” (Waefeso 6:18).

“Salini kila wakati!” Ni lazima tuwaombee kila wakati, watoto wa jamaa zetu na wa majirani. Ni lazima tuwaombee watoto wa marafiki zetu na marafiki wa watoto wetu. Ni lazima pia tuwaombee watoto walioko makanisani mwetu. Yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo tunapaswa kuombea sasa na kila wakati kwa ajili ya watoto wetu. (Pengine utataka kusoma vifungu vifuatavyo ulivyopewa pamoja na mambo ya kuombea.)

- ♦ Kutambua upendo wa Mungu na wapate kumpokea Kristo wakati wangali wadogo
- ♦ Kukua katika sehemu nne zilizotajwa katika Luka 2:52 (kimwili, kimawazo, kiroho na kijamii)
- ♦ Kutamani kumpendeza Mungu – 2 Wakorintho 5:9
- ♦ Kuchukia dhambi – kutambua dhambi na kukabiliana na matokeo ya dhambi wanapoasi
- ♦ Kuwalinda kutokana na mwovu
- ♦ Kuombea kupata marafiki wema na kwa ajili ya wenzao
- ♦ Kuwa na tabia nzuri – Danieli 6:3-4
- ♦ Kuwaheshimu wengine, hasa watu wazima – 1 Petro 2:17
- ♦ Mafano wetu sisi – uaminifu kwa yote tunayofanya, kuwa watu wa kweli na kusema ukweli
- ♦ Kukuza karama na vipawa walivyo navyo

Kuwalea na kuwafundisha watoto ni jambo muhimu sana. Hatuwezi kuliacha. Mwombe Mungu akusaidie. Mwulize mume wako, mke wako au rafiki Mkristo kuomba pamoja nawe kila juma. Kumbuka kwamba sura ya mwisho inayohusu uwakili wako wa zawadi ya Mungu ya watoto bado haijaandikwa!



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili:

Siku ya 1) Yohana 15:1-17; Siku ya 2) Zaburi 127;

Siku ya 3) Luka 2:41-52; Siku ya 4) Waefeso 6:1-9;

Siku ya 5) Waefeso 6:10-20; Siku ya 6) 2 Timotheo 1:1-10;

Siku ya 7) 1 Samweli 1:19-28

Karibuni Nyumbani Kwangu Mkakae

Maandiko ya Biblia: Luka 10:38-41; Matendo 16:29-34

Kifungu cha Kukumbuka: *‘Namwomba Mungu . . . naye Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani. Namwomba mpate kuwa na mizizi na msingi katika mapendo’*
Waefeso 3:17

Ruthu alitembea katika mvua pole pole akirudi nyumbani baada ya kumtembelea rafiki yake. Akawaza, “Je, kwa nini ninamjali Elizabeth? Je, ninamwonea wivu? La! nimefurahi kwa ajili yake. Anapaswa kujivunia nyumba yake mpya. Ni kubwa na nzuri kuliko ile ya zamani. Hata kuna shamba nje ya nyumba hiyo ambapo anaweza kukuza mboga na pia watoto wake wanaweza kutumia wakati wa kucheza.”

Ruthu alikumbuka jinsi Elizabeth alipowakemea watoto wake walipoingia ndani kunywa maji. Hakutaka wachafue jikoni. Rafiki yake Ruthu alijua jinsi ya kutunza nyumba, lakini yeye hakuwa hivyo.

Ruthu alikumbuka pia swali alilimwuliza kuhusu mahali pa kukutania kwa Ushirika wa Wanawake. Walipanga kukutana nyumbani kwa Elizabeth, lakini aliwaomba wakutanie nyumbani kwa Ruthu. Alitaka kungojea mpaka baada ya mvua kwisha. Hakutaka mkeka wake mpya alionunua uchafuke.

Je, umewahi kumfikiria rafiki yako jinsi hiyo baada ya kupata kazi au nyumba nzuri? Huwa tunasema kwamba tumebahatika wakati jambo jema linapotendeka kwetu. Mwanamke mmoja Mkristo alimsahihisha rafiki yake kwa kumwambia, “La, wewe umebarikiwa.”

Je, unakumbuka Yakobo 1:17? “Kila kipaji chema na kila zawadi kamilifu hutoka _____; hutoka kwa _____, Muumba wa mianga.” Je, unafikiri kwamba Elizabeth alimshukuru Mungu kwa nyumba yake mpya? Je, anaonyesha kuwa wakili mwema wa zawadi aliyopewa?

“Wapokeeni Wageni”

Kuna watu katika ulimwengu huu ambao hawana mahali pa kuita nyumbani kwao. Lakini, pengine ikiwa unasoma kitabu hiki una mahali ambapo unajua utaenda kulala usiku wa leo. Una mahali ambapo unaweka vitu unavyotumia kila siku na vitu unavyo thamini.

Nyumba zetu zimejengwa na vifaa tofauti. Nyumba moja anaweza isigharimu pesa zo zote hali nyingine inaweza kugharimu mamilioni

ya pesa. Pengine umeishi katika nyumba hiyo tangu utotoni au umeishi hapo kwa muda mfupi. Biblia inafundisha kwamba haijalishi jinsi nyumba yako ilivyo kubwa, salama au nzuri. Mungu anataka tuitumie kufanya kazi yake.

Biblia inasema wazi kwamba Wakristo wanapaswa kushiriki nyumba zao na watu wengine. Hebu tusome vifungu vifuatavyo ambavyo vinatukumbusha jambo hili na tukamilishe sentenzi zifuatazo.

- ♦ *Warumi 12:13* Tunapaswa _____ watu wa Mungu na kuwapokea wageni kwa ukarimu.
- ♦ *Tito 1:8* Ni lazima kiongozi wa kanisa awe mkarimu na _____ mambo mema.
- ♦ *1 Petro 4:9* Tunapaswa kuwa wakarimu bila _____.

Tutakuwa mawakili wema ikiwa tutatumia nyumba zetu kwa njia hii. Hebu tusome pia 1 Petro 4:10.

“Walimchukua Kwao”

Biblia inazungumzia kuhusu watu wengi waliotii amri ya Mungu na kuwakaribisha watu nyumbani kwao. Hebu tusome visa viwili katika Agano la Kale na tujibu maswali yafuatayo:

- ❖ *1 Wafalme 17:8-16* Je, mwanamke huyu alikuwa tajiri? Je, alitumia kile alichokuwa nacho kumtumikia Mungu?
- ❖ *2 Wafalme 4:8-10* Je, mwanamke huyu alikuwa tajiri? Je, alitumia kile alichokuwa nacho kumtumikia Mungu?

Agano Jipya linazungumzia pia wakati ambapo Wakristo walitumia nyumba zao kwa jina la Mungu. Someni na mjadiliane vifungu vifuatavyo:

- ❖ *Matendo 16:11-15* Je, Lydia alikuwa Mkristo kwa muda mrefu alipomkaribisha Paulo na kundi lake nyumbani kwake? Je, unafikiri alikuwa akitii sheria ya ukarimu au alikuwa akimtumikia Mungu?
- ❖ *Matendo 18:1-4, 24-26* Akila na Prisila walikuwa Wakristo waliokomaa walipohamia Korintho. Je, walitumiaje nyumba yao mpya?

Akila na Prisila walilazimika kuondoka Italia, lakini waliruhusu shida yao kuwa baraka. Je, Yesu alisema nini katika Matendo 1:8? (Mwambia mmoja wao aseme au asome kifungu hiki.)

Watu hawa walitumia kuhama kwao kama njia ya kushuhudia katika sehemu ngeni ambayo ilikuwa baadhi ya mwisho wa dahari. Makanisa mengi yameanzishwa na kukuzwa na Wakristo ambao wamehamia mahali ambapo hakuma kanisa au kuna kanisa dhafu.

“Alikuwa Anashughulika na Mambo Mengi”

Kuna wakati ambapo Wakristo watawakataa wageni nyumbani kwao. Huwa tunajishughulisha sana kuwatumikia wengine mpaka tunakosa nafasi ya kuwa na jamaa yetu wala kutimiza mahitaji yao. Kutakuwa na wakati ambapo Mungu atatuhitaji tumtumikie sehemu zingine mbali na nyumbani kwetu. Ikiwa tuna wakati wa kusoma neno lake na kuomba, Roho Mtakatifu atatuongoza kujua jinsi ya kutumia vizuri wakati wetu, nyumba na vipaji vyetu.

Ni lazima kukataa kwetu kutokane na hitaji la kutaka kutukuza jina la Mungu wala si letu wenyewe. Hebu tusome hadithi ya wanawake wawili ambao walifanya mambo tofauti katika nyumba moja. (Soma Luka 10:38-42.)

Je unaeleza kuhangaika kwa Martha? Wageni wake walihitaji kula. Walihitaji mahali pa kukaa. Mahitaji yao yalikuwa ya kweli, lakini shida ilikuwa kutimiza mahitaji yao. Martha, kama sisi, alikuwa akijaribu kufanya mambo mengi wakati mmoja. Pia, alikuwa anashughulikia mambo ambayo hayastahili.

“Afadhali Mlo wa Jioni wa Mchicha”

Mwanamke mmoja Mkristo alisema hivi, “Nimejifunza kuthamini Mithali 15:17: ‘Afadhali mlo wa jioni wa mchicha na upendo, kuliko karamu ya nyama nono pamoja na taabu.’ Nimejifunza kwamba wageni wengi huhitaji kala, lakini hiyo si sababu yao ya kukutembela. Huja kwako kuzungumza na kufurahi pamoja nawe au kuwa na mgeni mwingine. Inatosha tu kuwapatia mkate na cahi.”

Martha alichagua kukaribisha na kuwatunza wageni. Mariamu alichagua kukaa na kusikiliza mafundisho ya Yesu. Kuna wakati ambapo tunataka kuwatuza wageni kwa njia zote mbili. Ni lazima tujifunze jinsi ya kuwatunza wageni wetu lakini kwa njia rahisi. Kisha tutakuwa na nguvu ya kuweza kufurahia pamoja nao. Tutakuwa na wakati wa kuwasikiliza na kuwafanya kujiona wameheshimiwa.

Tunaweza pia kuwa na shughuli nyingi za kanisa mpaka tukose wakati wa kumheshimu Mungu. Tunaweza pia kujishughulisha sana na kazi ya Mungu mpaka tunachoka kuweza kuabudu. Tunaweza kuwajali sana watu wengine mpaka tunakosa wakati wa kufurahia ibada kama Wakristo wengine. Jibu ni rahisi sana. Ni lazima tusome neno la Mungu na kuomba kila siku. Hatupaswi kuwa na kazi nyingi mpaka tuanze kutafuta na kungojea mwongozo wa Mungu.

“Walikutana Katika Nyumba Zao”

Siku za kwanza baada ya Yesu kurudi mbinguni zilikuwa ngumu sana kwa Wakristo wa kwanza. Walijaa hofu na woga. Wengi

walikabiliwa na dhihaka hata kifo kwa imani yao. Lakini pia, walifurahi na kumwona Mungu akitenda kazi kwa njia ya ajabu. Hebu tusome baadhi ya Wakristo hawa wa kwanza katika Matendo 2:43-47.

Je, chanzo cha furaha ya watu hawa kilikuwa nini? Ilitokana na kumtumikia na kumtii Mungu kwa kikamilifu. Ilitokana na kuwa na moyo mkarimu wa kumtukiza na kumshukuru Mungu. Ilitokana na kuwa na ushirika na waamini wengine.

Matendo 4:32-36 inaanza hivi, “Jumuiya yote ya waumini ilikuwa moyo mmoja na roho moja.” Vifungu hivi vinazungumzia zaidi juu ya furaha ya Wakristo wa kwanza. Vinazungumzia pia jinsi Mungu alivyobariki ushuhuda wao kwa ulimengu uliowazunguka. (Soma Matendo 4:32-36.)

Je, ulimwengu wetu ungekuwa vipi ikiwa kila Mkristo angefuata mfano wa Wakristo hawa wa kwanza? Je, kanisa letu lingekuwa vipi? Ni lazima kila mmoja wetu ajiulize: Je, mimi ni wakili wa aina gani nikilinganishwa na Wakristo hawa? Je, ninapaswa kutoa na kufanya kiasi gani? Je, nyumba yangu inajulikana kuwa nyumba ya Mkristo? Je, wale ambao hawahudhurii kanisa wanaweza kuja nyumbani kwangu kujifunza Biblia au kuwatuma watoto wao kuja kujifunza Biblia nyumbani kwangu?

Kiongozi: Hebu tusome Kumbukumbu la Torati 11:19 na Matendo 16:29-34. Sisi kama mawakili wema ni lazima tutumie nyumba zetu kwa kufundisha na kuwaambia wengine juu ya upendo na wokovu wa Mungu. Tunaweza kuhakikishiwa kwamba tutajua furaha ambayo ilikuwa nyumbani mwa mlinzi wa gereza.

Ni lazima tukumbuke kwamba, sisi kama Wakristo hatuwezi kusema, nitatumika wakati nina nyumba nzuri, sahani nyingi au wakati watoto wangu wamekuwa wakubwa. Mungu anajua upungufu wetu. Anajua pia kile anachoweza kufanya tunapomruhusu kufanya kazi kupitia kwetu. Ombi letu linaweza kuwa Kifungu cha Kukumbuka cha leo: *‘Namwomba Mungu naye Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani. Namwomba mpate kuwa na mizizi na msingi katika upendo’* (Waefeso 3:17).



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Soma kwa makini maneno ya Yesu katika Mathayo 25:31-46 kila siku juma hili. Omba na umwulize Mungu afungue macho yako kwa nafasi ulizonazo kwa kumtumikia. Mwombe akuonyeshe njia mpya ya kuwaambia wengine juu ya upendo na wokovu wake nyumbani mwako.

Somo la Kumi na Moja

Wakili Mwema wa Karama za Kiroho

Maandiko ya Biblia: Warumi 12:6-8; 1 Wakorintho 12:4-10; Waefeso 4:11; 1 Petro 4:10-11

Kifungu cha Kukumbuka: *“Kila mmoja anapaswa kutumia kipaji alichojaliwa na Mungu kwa faida ya wengine kama wakili mwema wa zawadi mbalimbali za Mungu.”*
1 Petro 4:10

Yakobo alishanga alipofika kanisa wakati wa ibada ya mazishi ya baba yake. Mamia ya watu walikuwa ndani na nje ya kanisa hilo dogo. Imekuwaje hivyo? Baba yake hakuwa mtu anayejulikana wala mtu mashuhuri. Alikuwa mchungaji wa kanisa dogo katika eneo hilo.

Mwinjilisti anayejulikana sana alihubiri katika ibada hii. Alisema jinsi rafiki yake, baba yake Yakobo, alimhimiza kuhubiri. Rafiki yake alivyoandamana naye katika safari zake za kwenda kuhubiri

Yakobo alisikia wakati huu wa ibada na siku zilizofuatia neno hili kuhimiza likirudiwa tena na tena. Watu walisema mambo tofauti, lakini wote walisema sentenzi moja tu, “Maisha yangu yamebadilika kwa sababu ya kuhimizwa na baba yako.”

Mtu mmoja akasema, “Baba yako alinihimiza kwenda chuo kikuu. Nilipoona kwamba haiwezekani, alinisaidia kuona jinsi inavyo wezekana. Aliniandikia mara kwa mara nilipokuwa chuoni kunihimiza.”

Mwanamke mmoja aliandika hivi, “Mume wangu alikuwa wakati watoto wangu walipokuwa bado wadogo. Baba yako alinisaidia kupata kazi. Alinitembelea kazini kuniona na kunihimiza. Alirudia maneno ambayo mwinjilisti alisema wakati wa ibada, “Alikuwa na karama ya kiroho ya kuhimiza na aliitumia kwa manufaa ya watu wake.”

“Nitatia Roho Yangu Ndani Yako”

Wakati wa Agano la Kale, Mungu hakumpa kila mtu roho wake ambaye alimtumikia na kumtii. Aliwapa tu wanaume na wanawake wachache ambao aliwachagua. Viongozi na manabii hawa waliochaguliwa waliwafanyia kazi watu wake wote kwa nguvu na uongozi wa Roho.

Watu wa Mungu hawakuamua kila wakati kumtumikia na kumtii. Dhambi zao ziliwafanya wateseke na kutekwa kwa nchi yao na

mataifa mengine. Nabii Isaya aliaandika kwamba Mungu aliwapenda watu wake na akawakomboza kutoka kwa matokeo ya dhambi zao, lakini wao waliendelea kufanya dhambi. Wakati ulifika “wakaihuza roho yake takatifu. Basi, Mungu akageuka, akawa adui yao; yeye mwenyewe akapigana nao” (Isaya 63:10).

Mungu aliendelea kuwapenda watu wake na alitaka kuanza uhusiano mpya nao. Hebu tusome yale aliyomwambia mmojawapo wa manabii wake aliowachagua katika Ezekiel 36:26-31.

“Msaidizi, Roho Mtakatifu”

Siku hizi, “tunaishi chini ya agano na uhusiani mpya na Mungu, wala si lile agano la wakati wa Agano la Kale. Tuna mfano wa Yesu Kristo wa kufuata na Roho Mtakatifu aliye ndani yetu hutufundisha na kutuongoza” (Somo la Tatu, ukurasa wa 16). Yesu kabla ya kurudi kwa baba yake, aliambia wanafunzi wake, “Nami nitamwomba Baba naye atawapeni Msaidizi mwingine, atakayekaa nanyi milele. Yeye ni Roho wa ukweli” (Yohana 14:16-17). Je, hii inakukumbusha ahadi ya Mungu katika Ezekiel 36?

Roho Mtakatifu hufanya kazi maishani mwetu kwa njia tofauti. Soma vifungu vifuatavyo na uanduke kila kifungu mbele ya kila kazi yake: Yohana 14:26; Yohana 16:7-8; Matendo 1:8; Warumi 8:13; Warumi 8:15-16; 1 Wakorintho 12:1, 11; Waefeso 1:13-14.

- ♦ Hutusaidia kuacha matendo yetu ya dhambi (Mfano) Warumi 8:13
- ♦ Huwafanya Wakristo kuwa wana wa Mungu _____
- ♦ Hutufundisha na kutukumbusha mafundisho ya Yesu _____
- ♦ Huthibitisha wokovu wetu _____
- ♦ Huwajaza Wakristo na Nguvu _____
- ♦ Huwaonyesha watu dhambi zao _____
- ♦ Humpatia kila Mkristo karama tofauti _____

“Kwa Faida ya Wengine”

Kifungu cha Kukumbuka cha leo, 1 Petro 4:10, kinasema, “Kila mmoja anapaswa kutumia kipaji alichojaliwa na Mungu kwa faida ya wengine kama wakili mwema wa zawadi mbalimbali za Mungu.” Wakati wa Agano la Kale, Mungu alichagua tu watu wachache kufanya kazi yake. Siku hizi anawaita watoto wake wote kumfanyia kazi. Hii sehemu ya wajibu wa uhusiano mpya. Ni lazima kila mmoja wetu atumie kipaji (karama) chake kwa faida ya wengine wote.

Paulo aliandika, “Vipaji vya kiroho ni vya nama nyingi, lakini Roho avitoaye ni mmoja. . . . Kila mtu hupewa mwangaza wa Roho kwa faida ya wote” (1 Wakorintho 12:4, 7). Baadaye katika barua hii, Paulo anasema kwamba hakuna mtu anayepewa vipaji vyote vya kiroho lakini, kila mwamini hupokea angaa kipaji kimoja. Alifundisha pia kwamba hakuna kipaji ambacho ni bora zaidi kuliko kingine.

Sisi ni sehemu ya kundi linaloitwa mwili wa Kristo. Wakati mwingine kundi hili huitwa kanisa. Ili kundi letu lifanye kazi, ni lazima kila mtu atumie kipaji chake au vipaji kwa kikamilifu. Hebu tusome Waefeso 4:12, 15-16.

“Roho Humpa . . . ”

Paulo aliandika katika Warumi 12:6, “Basi, tunavyo vipaji mbalimbali kadiri ya neema tuliyopewa.” Paulo anaanza kutaja vipaji vya kiroho katika kifungu hiki na vile vinavyofuata.

- ♦ *Kipaji cha unabii na kunena kwa lugha au kuhubiri ujumbe wa Mungu.*
- ♦ *Vipaji vya utumishi, kufundisha, kufariji na kutoa.*
- ♦ *Kipaji cha mamlaka na uongozi*
- ♦ *Kipaji cha kuonyesha ukarimu na huruma*

Wamini wa Korintho walikuwa na maswali kuhusu vipaji vya Kiroho. Paulo aliwaambia mambo haya alipowajibu katika 1 Wakorintho 12:

- ♦ *Vipaji vya hekima, elimu na imani*
- ♦ *Kipaji cha kuponya na kufanya miujiza*
- ♦ *“Kipaji cha kubainisha vipaji vitokavyo kwa Roho na visivyo vya Roho”*
- ♦ *Vipaji vya kusema kwa lugha na cha kuzifafanua*

Paulo katika barua yake kwa Wakristo wa Efeso, alijumlisha vipaji vingi pamoja na kazi zao maalum. “Wengine aliwajalia wawe mitume, wengine manabii, wengine wawe waeneza injili, wengine wachungaji na waalimu. Alifanya hivyo apate kuwatayarisha watu wote wa Mungu kwa ajili ya kazi ya huduma ya Kikristo ili kuujenga mwili wa Kristo” (Waefeso 4:11-12).

“Wakili Mwema wa Zawadi Mbalimbali za Mungu”

Ikiwa tunataka kuwa “wakili mwema wa zawadi mbalimbali za Mungu” (1 Petro 4:10), ni lazima tutake kuwa wasimamize. Je,

unajua karama au vipaji ambavyo umepewa na Roho Mtakatifu? Je, unajua jinsi ya kugundua kipaji chako?

Roho Mtakatifu wa Mungu hutupatia vipaji vya kiroho. Anaweza pia kutusaidia kutambua kipaji tulicho nacho. Hutusaidia kupata majibu tunapoomba na kusoma Biblia. Paulo aliandika kwamba, “Salini daima, mkiomba msaada wa Mungu. Salini kila wakati kwa nguvu ya Roho” (Waefeso 6:18). Je, unakumbuka Waebrania 4:12? “Neno la Mungu ni hai na lina nguvu; ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili.” Roho Mtakatifu anaweza pia kuwaongoza Wakristo wengine kusaidia. Rafiki zako Wakristo wanaweza kujua kipaji chako.

Kila mtu huzaliwa na uwezo fulani kama kuimba, kuchora au kusimulia hadithi. Uwezo huu unaweza kutumiwa jinsi tunavyotumia kipaji cha kiroho. Mtu mwenye uwezo wa kufundisha watoto anaweza kuwa na kipaji cha kufundisha ujumbe wa Mungu. Mtu anayependa kupika anaweza kutumia kipaji hiki kusaidia wengine. Je, unatumiaje uwezo maalum ulionao kumtii na kumtumikia Mungu? Ikiwa unajua uwezo wako, unaweza kukusaidia kutambua kipaji chako cha jiroho.

Kiongozi: Wakati mwingine watu huogopa kutumia vipaji vyao vya kiroho. Huogopa kwamba Mungu atawaambia wafanye jambo gumu zaidi. Pengine huhofia yale ambayo watu wengine watasema. Soma 1 Petro 4:11.

Je, tunapaswa kutumika kwa nguvu zetu wenyewe? La! Mungu atatupatia nguvu tunazohitaji kufanya kazi yake. Je, tunatumia vipaji vyetu ili tusifiwe na watu wengine? Tunapaswa kuvitumia kwa manufaa ya watu wengine, lakini vinapaswa kutumiwa ili “Mungu apewe sifa kupita kwa Yesu Kristo.”

Paulo alimwambia Timotheo, “Usiache kukitumia kile kipaji cha Kristo ndani yako” (1 Timotheo 4:14). Kabla ya kuomba, hebu jibu maswali haya moyoni mwako: Je, ninapuza au ninatumia vizuri kiapji changu? Je, ninahitaji kukuza kipaji changu? Je, kuna yale ninayofanya ambayo si kwa wema wa wengine kwa sababu mimi si wakili mwema wa kipaji changu cha kiroho?



Vifungu vya Biblia vy a Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Warumi 12:1-13; Siku ya 2) 1 Wakorintho 12:1-11; Siku ya 3) 1 Wakorintho 12:12-31; Siku ya 4) Waefeso 4:4-16; Siku ya 5) 1 Petro 4:7-11; Siku ya 6) Yohana 14:15-31; Siku ya 7) Yohana 16:5-15

Ujumbe wa Kristo Ukae Moyoni Mwako

Maandiko ya Biblia: Matendo 18:24-28; 1 Wakorintho 2:1-5

Kifungu cha Kukumbuka: *“Lakini mtukuzeni Kristo kama Bwana mioyoni mwenu. Mwe tayari kumjibu yeyote atakayewaulizeni juu ya matumaini yaliyo ndani yenu.”*
1 Petro 3:15

Amosi, alipokuwa akitembea na mkewe kwenda nyumbani alisema, “Leo ningekaa tu nyumbani. Mnenaji wa leo anapaswa kujifunza mambo fulani. Nilimtarajia kuwa mtu mwenye elimu na mwerevu. Mimi ninajua mengi zaidi kuliko yeye.

Anna akamjibu, “Alikuwa tu mtu mashuhuri mwenye mavazi ya bei ghali ambaye alijionyesha jinsi anavyojua mengi. Je, alifiri kwamba sisi ni wajinga? Tunajua mengi kuhusu Yesu kuliko anavyojua.”

Akila naye akiwa njiani kwenda kanisani aksema, “Mnenaji wa leo alifahamu sana Agano la Kale. Alikuwa mweruvu sana na mwalimu mzuri. *Hapaswi* kujua yale yaliyompata Yesu.”

Prisila akamjibu, “Alinena kwa ujasiri mkubwa. Hebu turudi kanisani na tumwalike nyumbani kwetu leo. Mungu anaweza kumtumia sana ikiwa atamwelewa Yesu vizuri na maisha yake!”

Hadithi iliyo hapo juu haiko katika Biblia, lakini tunajua kwamba Akila na Prisila hawakupoteza wakati wao wakimlalamikia Apollos. Walimsaidia walipojua sehemu ya Yesu katika mpango wa Mungu wa wokovu wa mwanadamu. Walimkaribisha nyumbani kwao na wakamfundisha. Biblia inasema kwamba Apollos alikuwa wakili mwema wa yale aliyojifunza. Aliheshimiwa na kuthaminiwa kama mwalimu wa Wakristo wapa. Hebu tusome Matendo 18:24-28 na 1 Wakorintho 3:5-6.

Tumejifunza kwamba Wakristo wanapaswa kuwa mawakili wema wa vipaji vyote vya Mungu. Tuisahau kujumlisha kile kipaji muhimu ambacho tumepokea. Ni lazima tuwe mawakili wema wa ujumbe wa upendo na wokovu wa Mungu. Tunapata ujumbe wake katika Biblia na tunawaambia wengine kwa kuwashuhudia.

“Akianzia na Sehemu Hiyo ya Maandiko Matakatifu”

Je, umewahi kuogopa kujibu swali kwa sababu haujui? Wakristo wanapoteza nafasi nyingi ya kushuhudia na kuwafanya watu kuwa

wanafunzi kwa sababu wanaogopa kwamba hawajui. Hatupaswi kujua yote. Tuna kitabu ambacho kina majibu yote. Soma vifungu vifuatavyo na ujibu maswali haya:

- ❖ *Mathayo 4:14* Je, Yesu alimkariria nini Shetani?
- ❖ *Matendo 8:30-35* Je, Filipo alitumia Maandiko kusimulia Habri Njema ya nani?
- ❖ *Matendo 17:11* Je, kwa nini watu walijifunza Maandiko?
- ❖ *Wakolosai 3:16* Je, neno la Mungu linapaswa kuishi wapi?
- ❖ *Mathayo 22:29* Je, Yesu angesema maneno haya juu yako?

Ni lazima tutumie Biblia ikiwa tunataka kujua ni nini. Ni lazima tuisome. Ni lazima tujifunze. Ni lazima tuikariri. Wakristo wengi hufungua tu Biblia yao katika ibada wakati wa Jumapili. Je, kungefanyika nini ikiwa ungekula tu chakula siku ya Jumapili asubuhi kwa masaa mawili? Chakula cha kiroho ni muhimu kama chakula cha kimwili. Hatuwezi kukua kama Wakristo ikiwa hatuli chakula cha neno la Mungu. Hatuwezi kuwa sehemu inayozaa na kuwaleta Wakristo wapya ikiwa hatujui neno al Mungu.

“Maandiko Yote . . . Yanafaa”

Sisi kama watoto ambao wakati mwingine hukataa kula, ni lazima tukumbushwe kwa nini Neno la Mungu linapaswa kuwa sehemu muhimu ya maisha yetu. Tayari tumejifunza sababu moja katika Somo la Tatu, ukurasa wa 16. Sisi kama Wabatisti “tunaamini kwamba mafundisho ya Yesu katika Agano Jipya yanapaswa kuwa mwongozo wetu katika imani na matendo. Hii haifanyi Agano la Kale liswe muhimu. Ni lazima tujifunze Biblia yetu yote ikiwa tunataka kujua na kuelewa Mungu wetu na mipango yake kwa watu wake.”

Biblia ilikuwa mwongozo wetu kabla ya kuwa Wakristo. Je, mtu alitumia vifungu kukuonyesha kwamba wewe ni mwenye dhabmi? Je, ulipata wapi yale uliyopaswa kufanya ili uwe Mkristo? Mpango mmoja wa wokovu na baadhi ya vifungu hivi unapatikana nyuma ya kitabu hiki. Hebu tusome 2 Timotheo 3:15-17.

“Neno Lako ni Taa ya Kuniongoza”

Mungu anaweza kufanya miujiza, lakini haweki ufahamu wa Biblia mioyoni na katika akili zetu wakati tunapokuwa Wakristo. Hutupatia roho Mtakatifu kama msaidizi wetu. Roho Mtakatifu hutusaidia kuelewa ukweli wa Mungu tunaposoma Biblia. Hutufundisha na kutusaidia kukumbuka yote ambayo Yesu alifundisha. (Soma Yohana 14:16-17, 26.)

Zaburi 119:105 inasema, “Neno lako ni taa ya kuniongoza, na mwanga katika njia yangu.” Hii ni kweli, Lakini ni lazima tumpatie Roho Mtakatifu wakati wa kutuongoza na kutusaidia. Tunafanya hivyo kwa kusoma Bibla na kuomba. Ni lazima tuzungumze na Mungu kuhusu yale tunayosoma na ni lazima tuwe na wakati wa kusikiliza majibu yake.

Ni lazima tujifunze Biblia na watu wengine. Mekanisa mengi hufanya hivi Jumapili asubuhi. Mekanisa mengine hayajifunzi na husema kwamba vitabu vya kujifunzia ni ghali sana. Je, nyama kilo moja ni shilingi ngapi? Je, nyama hii inaweza kuliwa na watu wazima ishiri kwa majuma kumi na matatu? Vitabu vingi vya kujifunza Bibla hugarimu chini ya bei ya kilo moja ya nyama. Kitabu kimoja kinaweza kutumiwa *kuwalisha* kundi kubwa la watu kila Jumapili kwa miezi mitatu!

“Neno Lako Moyoni Mwangu”

Zaburi 119:11 inasema, “Nimeshika neno lako moyoni mwangu, nisije nikakukosea.” Hatuweza kubeba Biblia zetu mkononi kila wakati, lakini tunaweza kubeba neno la Mungu moyoni mwetu. Tunapokariri vifungu, vitakuwa moyoni mwetu vikingojea kuwa kama ukumbusho, mfariji na wakati mwingine kama jibu. Tunaweza pia kutumia vifungu tulivyo kariri kama ukumbusho, mfariji na jibu la kuwaambia wengine.

Mungu alisema katika Kumbukumbu la Torati 6:4-7 yale anayowatarajia watu wake kufanyia neno lake. Soma vifungu hivi na ukamilishe sentenzi hizi:

- ❖ _____ watoto wenu.
- ❖ Waambieni mwapo _____ na mwapo safarini.
- ❖ Semeni mnapolala na mnapo _____.

Kumbukumbu la Torati 6:8 inatuhimiza kwamba tuandike neno la Mungu kwenye sehemu muhimu nyumbani kwetu. Je, kuna vifungu kwenye kuta za nyumba yenu? Vifungu hivi vinavyopatikana katika Kumbukumbu la Torati vinaeleza jinsi ya kushuhudia na kuwaambia wengine kila siku juu ya imani yetu. Je, majirani zako wanajua kwamba Mungu ni Baba na Bwana wako? Je, wanaona amani na furaha maalum uliyo nayo?

“Sikuwahubiria Siri ya Ujumbe . . . Kwa Ufasaha wa Lugha”

Ni lazima wakili mwema wa ujumbe wa Mungu ajihusishe zaidi mbali na kujua au kutumia ujumbe wa Mungu kila siku. Ni lazima tuwaambie wengine ujumbe huu. Washiriki wengi hutarajia viongozi wao wa kanisa kufanya mipango yote ya kwenda kushuhudia. Wanajisikia kwamba hawajui ya kutosha, hawana wakati wa kutosha, au watafanya kazi mbaya. Yereimia alikuwa nabii mkuu. Mungu

alipomwita kufanya kazi yake, Yeremia alimwambia, "Aa! Bwana Mwenyezi Mungu, mimi sijui kusema." Soma Yeremia 1:6-9.

Katika 1 Wakorintho 2:1-5, Paulo ameandika jinsi alivyo hubiri ujumbe wa Mungu, "Sikuwahubiria siri ya ujumbe wa Mungu kwa ufasaha wa lugha, au kwa hekima ya binadamu. . . Nilipokuja kwenu nilikuwa dhaifu, natetemeka kwa hofu nyingi." Paulo hakuwa akiomba msamaha. Alikuwa anawakumbusha waamini kwamba aliwaletea ujumbe wa Mungu naye aliwaambia kwa nguvu za Mungu, wala si nguvu zake mwenyewe.

Ikiwa tutangoja mpaka tuwe tayari kunena ujumbe wa Mungu wa wokovu, hatutanena kamwe, au tusinene! Ni lazima tutambue kwamba sisi ni watumwa. Jinsi alivyomfanyia Yeremia, *Mungu atatupatia maneno ya kusema*. Ni lazima tuseme ujumbe wake kwa nguvu zake, na sio zetu wenyewe.

Hii haimaanishi kwamba tusijitayarishe na tujitoe kwenda kushuhudia. Soma Kifungu cha Kukumbuka cha leo, 1 Petro 3:15. Je, tunawezaje kuwa tayari kila wakati kusema ujumbe wa upendo na wokovu wa Mungu? Tunaweza kuanza kwa kukariri mojawapo ya mpango wa wokovu na vifungu vyake!

Kiongozi: Wakolosai 3:16 "Ujumbe wa Kristo na ukae ndani yenu." Wakati ujumbe wa Mungu unapokaa mioyoni mwetu, tutataka kuwaambia wengine. Tutataka kuwa wakaili mwema wa kipaji tulichopokea kutoka kwa Mungu.

Paulo alimwambia Timotheo kwamba, "Nakuamuru . . . hubiri huo ujumbe, sisitiza kuutangaza. . . karipia, onya na himiza watu ukiwafundisha kwa uvumilivu wote" (2 Timotheo 4:1-2). Sisi wote hatupewi kipaji cha kiroho cha kuhubiri na kufundisha, lakini sisi sote tunao wajibu wa kuwaambia watu juu ya upendo na wokovu wa Mungu.

Hebu tusome Waebrania 5:11-14 kabla ya kufunga kwa maombi. Je, sisi ni Wakristo waliokomaa kiroho ambao tunaweza kuruhusu Biblia itukaripie, ituonye na kutuhimiza? Je, tumejifunza jinsi ya kutumia neno la Mungu kwa kuwakaripia, kuwaonya na kuwahimiza wengine kwa uvumilivu? Hebu tuombe kwamba tutakuwa mawakili wema wa ujumbe wa Mungu.



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Zaburi 119:1-24; Siku ya 2) Zaburi 119:25-48; Siku ya 3) Zaburi 119:49-72; Siku ya 4) Zaburi 119:73-104; Siku ya 5) Zaburi 119:105-128; Siku ya 6) Zaburi 119:129-152; Siku ya 7) Zaburi 119:153-176

Mungu Afanye Mabadiliko

Maandiko ya Biblia: Luka 16:1-15; Warumi 12:1-2

Kifungu cha Kukumbuka: *“Kwa maana Roho tuliypewa na Mungu si wa kutufanya tuwe waoga; sivyo, ila ni Roho wa kutujalia upendo na nidhamu.”* 2 Timotheo 1:7

Mwanamke yule akafikiria, “Watu wangu wamepatwa na shida nyingi. Tumemwasi Mungu sana, lakini leo ni tofauti. Tunajenga pamoja nyumba hii kumtukuza Mungu jinsi anavyotaka.”

Wanawake wengi walikuwa wamevaa vipuli vya dhahabu na fedha, ngozi za wanyama na ushanga. Vyote vingetumiwa kumjengea Mungu nyumba nzuri mahali panapofaa. Akawaza, “Sisi huwa wachoyo sana, lakini tayari tumepewa vitu vingi zaidi ya vile vinavyo hitajika kumaliza kazi hiyo.”

Mwanamke huyu aliangalia wakati wajenzi bora, washonaji na wahunzi walivyotayarisha nyumba ya Mungu. Akawaza, “Kazi yao ni nzuri sana, lakini nimeshangazwa sana na tabia yao. Wanafanya kazi pamoja bila wivu wala majivuno, wanafanya kazi pamoja na kuwafundisha wengine jinsi ya kuwasaidia!”

Watu walikuwa na furaha kila wakati kutumia uweza na mali waliyopewa na Mungu. Walikuwa wakifanya kazi pamoja kumpendeza na kumtumikia Mungu. Mwanamke huyo akasema, “Ahadi ya Mungu inatimia. Mambo makuu na ya ajabu yanafanywa ambayo hayajawahi kamwe kufanyika. Tunampendeza Mungu pamoja na kufanya kazi yake.”

Hadithi iliyo hapo juu haisimuliwi katika Biblia jinsi mwanamke huyu anavyowaza, lakini ni hadithi ya kweli. Sura ya mwisho ya Kutoka inazungumzia kuhusu wakati maalum, wakati watu wa Mungu walitumia mali zao, wakati, uwezo na maarifa kumtumikia Mungu kwa moyo, roho na akili zao zote.

“Itasababisha Watu Wengi Wamshukuru Mungu”

Tumejifunza katika kitabu hiki, kundi la mawakili wema wa zawadi za Mungu kwao. Hebu turudie vifungu hivi vinavyohusu Wakristo wa Kwanza:

- ❖ Matendo 2:43-47 “_____ wote waliendelea kuwa kitu kimoja na mali zao waligawiana. . . Kila siku _____ aliwaongezea idadi ya watu waliokuwa wakiokolewa.”

- ❖ *Matendo 4:32-35* “Jumuiya yote ya waumini ilikuwa _____ mmoja na _____ moja. . . naye Mungu akawapa baraka nyingi.”
- ❖ *2 Wakorintho 8:1-5* “Walikuwa wakarimu kadiri ya nguvu zao na hata _____ . . . Kwanza walijitolea wao wenyewe kwa _____.”
- ❖ *2 Wakorintho 8:12* “Maana ikiwa mtu ana moyo wa kusaidia, Mungu hupokea kila anachoweza kutoa; _____ zaidi.”
- ❖ *2 Wakorintho 9:6-15* “Kila mmoja, basi, na _____ kadiri alivyoamua, kwa moyo na wala si kwa huzuni au kwa kulazimishwa, maana Mungu _____ yule mwenye kutoa kwa furaha. . . Maana huduma hii takatifu mnayoifanya si kwamba itasaidia mahitaji ya _____ wa Mungu tu, bali pia itasababisha watu wengi wamshukuru _____.”

“Mungu Uwe Utukufu”

Watu wa Kutoka na waamini hawakujiita mawakili, lakini tunajua kwamba wao walikuwa mawakili. Walikuwa mawakili wema wa zawadi zote walizopewa na Mungu. Walizitumia kumtukiza, kumtumikia na kumtii. Walitumia zawadi hizi kufanya kazi yake. Waliweza kufanya mambo makuu kwa kumtegemea Mungu. (Soma Waefeso 3:20-21.)

Mambo mengi yalibadilikia wana wa Mungu kutoka wakati wa Musa na wakati Paulo alipoandikia waamini barua hizi. Mungu alileta njia mpya ya kumjua na kumtumikia kupitia kwa Mwanawe, Yesu Kristo. Hebu tusome Yeremia 31:33.

Lakini baadhi ya mambo mengine hayajabadilika. Tungali tunapaswa kumpenda Mungu kwa moyo, roho na akili zetu zote. Ni lazima tuchague kutumia zawadi zote alizotupatia kumheshimu, kumtumika na kumtii. Tungali na wajibu wa kutumia zawadi alizotupatia kufanya kazi yake.

Je, tunaweza kuwa watumishi wa Mungu na mawakili wema wa zawadi alizotupatia? Hatuwezi kwa nguvu zetu wenyewe, lakini tunaweza “kwa nguvu zake maishani mwetu.” Tunapotegemea nguvu za Mungu, anaweza kututumia na zawadi zetu kufanya kazi yake. Tunaweza kuwa mashahidi imara wa upendo na wokovu wake. Hebu tusome Waefeso 3:15-21 na Kifungu cha Kukumbuka cha leo, 2 Timotheo 1:7.

“Takatifu na Yenye Kupendeza”

Wakristo wengi wanaamini kwamba kwa nguvu za Mungu, wanaweza na watapaswa kufanya kazi yake na kuwa mawakili wema. Lakini, wengi hawategemei kutumia nguvu zake. Paulo, katika Waefeso

4:14 anaelezea baadhi ya Wakristo kama watoto. Hawaiti watoto wa Mungu wakati huu. Anawaita watoto kwa sababu hawajakua.

Paulo anatumia tuzidi “katika kila jambo kulingana na Kristo” (Waefeso 4:15). Je, tunakuaje na kuwa Wakristo waliokomaa? Je, tunaaminiwa vipi na kuwa mawakili na watumishi waaminifu? Hebu tusome yale ambayo Paulo alisema katika barua zifuatazo kwa Wakristo wanaokua.

- ❖ Warumi 12:1-2 “Bali Mungu afanye mabadiliko ndani yenu kwa kuzigeuza _____ zenu.”
- ❖ Waefeso 4:22-24 “Jirekebisheni upya _____ na katika zenu.”
- ❖ Wakolosai 3:12-17 “Ujumbe wa Kristo na ukae _____ pamoja na utajiri wake wote.”

Wakristo wengi hawajui furaha ya kumtumikia Kristo na kuwa mawakili wema wa zawadi zake. Hawajui “jinsi upendo wa Kristo ueneavyo kwa mapana na marefu, kwa kimo na kina” (Waefeso 3:18).

Wakristo wengi hutii amri za Mungu kama sheria. Hawatamani kumjua, kumtumikia na kumtii kwa moyo, roho na akili zao zote. Mungu anataka kila mmoja wetu kuwa mtoto wake, lakini anataka pia tuwe watoto walioku na kukomaa. Anataka hivyo ili jina lake litukuzwe. Anataka hivyo pia kwa sababu ni nzuri kwetu. Hebu tusome alivyowaambia manabii wake katika Isaya 48:18 na Yeria 29:11-13.

“Mungu Anajua Mioyo Yenu”

Yesu, katika *Mfano wa Wakili Mjinga*, alisimulia kuhusu wakili mwerevu na mwenye bidii. Wakili huyu alifanya kazi kwa faida yake mwenyewe, si kwa faida ya mwenye mali. Hebu tuangalie maneno ya Yesu katika Luka 16.

- ♦ Watu wachoyo na wenye tamaa mbaya hufanya kazi kwa *moyo, roho na akili* zao zote kutimiza mahitaji yao. Ni lazima wakili Mkristo amtumikie Mungu kwa nguvu kama hizo. (Soma Luka 16:1-8.)
- ♦ Mawakili Wakristo wana wajibu wa Kutumia *kila* nafasi wanayopata kumtumika Mungu, mwenye na anyeyepeana zawadi zote. (Soma Luka 16:9.)
- ♦ Wakili mwema atamtumikia bwana wake katika njia ndogo na kubwa. Ni lazima wakili mwema atunze vizuri mali *yote* ambayo bwana wake anamwachia kusimamia. (Soma Luka 16:10-12.)
- ♦ Mungu anajua mioyo yetu. Haoni tu *jinsi* tunavyomtumika. Anajua *kwa nini* tunamtumika. (Soma Luka 16:15.)

“Inayohitajiwa Katika Mawakili”

Tumejifunza katika kitabu hiki matakwa ya mawakili Wakristo. (Mwambia mmoja wao asome au aseme Kifungu cha Kukumbuka cha Somo la Pili, 1 Wakorintho 4:1-2.) Hebu turudie yale ambayo tumejifunza kwa kujibu kwa uaminifu maswali haya, kwa kutumia Biblia kama mwongozo wetu:

- ♦ Je, ninakubali kwamba mimi ni mali ya Mungu na vyote nilivyo navyo?
- ♦ Je, ninatamani kuwa wakili Mkristo mwema na mwaminifu wa zawadi zote nilizopewa na Mungu?
- ♦ Je, ninampenda na kumtumikia na kumtii Mungu kwa moyo, roho na akili zangu zote?
- ♦ Je, niko tayari kujitumia mimi na vyote nilivyo navyo kumtumika na kumtii Mungu kila wakati?
- ♦ Je, ninamkumbuka Mungu kwa mambo yote ninayofanya? Je, ninamruhusu aishi moyoni mwangu na kutawala kila matendo na mawazo yangu?
- ♦ Je, ninaomba kila wakati na kutafuta mwongozo na msaada wa Mungu?
- ♦ Je, kunao watu ambao wana mahitaji kwa sababu sijawahi kuwa wakili mwema wa mali na uwezo wangu?
- ♦ Je, ninatoa zaka na sadaka kwa sababu ninatii sheria au kwa sababu ninataka kumheshimu, kumtumikia na kumshukuru Mungu?
- ♦ Je, mimi ni wakili mwema wa kipaji changu cha kiroho? Je, ninatumia kipaji hiki kwa ajili ya wengine na kwa kujenga mwili wa Kristo?
- ♦ Je, ujumbe wa Mungu unakaa moyoni mwangu? Je, mimi ni wakili mwema wa ushuhuda wangu wa upendo na wokovu wa Mungu?

Kiongozi: *Sisi ni wafanya kazi pamoja na Mungu.* Sisi ni shamba lake, jengo na hekalu. Ni lazima tuwe waangalifu jinsi tunavyotumia vipaji tunavyopewa na Baba yetu wa mbinguni. Hebu tumalizie somo hili la uwakili kwa kusoma 1 Wakorintho 3:1-16. (Soma vifungu hivi.)

Kila Mkristo ni sehemu ya mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:27). Mungu anahitaji kila mmoja wetu kama sehemu ya mwili wa Kristo, kanisa, kufanya kazi yake. Hebu tuombe kwamba Mungu atatupata tukiwa watumishi waaminifu na mawakili wema wa vipaji vyote na miujiza yake.



Vifungu vya Biblia vya Kusoma Juma Hili: Siku ya 1) Wafilipi 2:1-11; Siku ya 2) Kutoka 31:1-11, 34:10; Siku ya 3) Kutoka 35:10-19; Siku ya 4) Kutoka 35:30-36:6; Siku ya 5) 2 Wakorintho 2:14-17; Siku ya 6) Kumbukumbu la Torati 10:12-22; Siku ya 7) Warumi 5:1-11

Mpango wa Mungu wa Wokovu

Vifungu vifuatavyo vya Biblia vinazungumzia **mpango wa Mungu wa wokovu** kwa wale ambao wamepotea. Vinaeleza ukweli ambao ni lazima mtu asikie na kukubali ili aokoze.

1) **Warumi 3:23** Ni lazima mtu huyo aelewe kwamba yeye ni mwenye dhambi na kwamba dhambi imemtenganisha na Mungu.

2) **Warumi 6:23** Ni lazima mtu huyo ajue kwamba mwenye dhambi amekabiliwa na mauti. Mungu hataki mtu ye yote atenganishwe naye. Anatoa zawadi ya uzima wa milele katika Yesu Kristo.

3) **Yohana 3:16** Mungu anatupenda na anatoa njia ya kutuwezesha kupata zawadi yake ya uzima wa milele. Ni lazima mtu amwamini Yesu ndipo apokee zawadi hii.

4) **1 Yohana 1:9** Ni lazima mtu akiri dhambi zake ndipo akubali mpango wa Mungu. Ni lazima atubu dhambi zake na amwombe Mungu msamaha. Ni lazima pia amwambie Mungu atawale maisha yake.

5) **Warumi 10:9-10** Ni lazima mtu huyo aamini kwamba Mungu amefanya kile alichohidi. Ni lazima mtu huyo aamini kwamba amesamehewa dhambi zake na amepokea karama ya Mungu ya uzima wa milele.

Baada ya kutumia vifungu hivi, mwulize mtu huyo kama anaamini kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zake. Mwulize kama yuko tayari kufuata mpango wa Mungu wa wokovu. Ikiwa mtu huyo anataka kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi, mwambie aombe. Mwongoze anapompokea Yesu maishani mwake. Mwongoze anapomwomba Mungu msamaha wa dhambi zake na kumtaka atawale maisha yake.